MEI 2025 | TOLEO LA 0005

>>>>>>>>>>>>>>Jarida la fahari ya

# DODOMA

## ZIARA YA MABALOZI ILIVYOTIKISA DODOMA








## DHAMIRA YA MHE. RAIS, WATANZANIA KUPATA HUDUMA YATIMIA KWA MKOA WA DODOMA



## VITUO VYA 'KILIMO ANGA' NCHINI, KUPATA NDEGE MPYA ZA KUDHIBITI VISUMBUFU VYA MIMEA



## DODOMA, FAHARI YA WATANZANIA.

**MHARIRI**
Francisca F. Mselemu

**WAANDISHI/WAPIGA PICHA**
Hellen M. Minja
Sizah Kangalawe
Sofia Remmi
Happiness Chindiye

**MSANIFU WA JARIDA**
Stephano H. Silaa



# SALAMU ZA MKUU WA MKOA

Wananchi wa Mkoa wa Dodoma, na wapendwa wote mlio ndani na nje ya Mkoa wetu,
Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi ya kuendelea kushuhudia maendeleo makubwa katika Mkoa wetu. Mwezi Mei huanza na Sikukuu ya Wafanyakazi. Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza sana wafanyakazi wote wa Mkoa wa Dodoma kwa juhudi zao kubwa na ushirikiano wao katika kuhakikisha maendeleo yanapatikana. Nikiwa Kiongozi wa Mkoa huu, ninatambua na kuthamini mchango wenu katika kujenga Mkoa wa Dodoma, Hongereni sana!
Kadhalika, Mwezi Mei tumesherehekea Siku ya Nyuki Duniani. Siku hii ilitupa fursa ya kutafakari umuhimu wa nyuki katika ikolojia yetu na uchumi wetu. Tunaendelea kuhamasisha ufugaji wa nyuki kwa njia endelevu ili kuongeza kipato kwa Wananchi wetu huku tukilinda mazingira.
Mwezi Mei ,2025 umekuwa mwezi wa baraka kwa Mkoa wa Dodoma kwa kufanikisha ziara kubwa, na ya kidiplomasia ya Waheshimiwa Mabalozi wanaoziwakilisha Nchi zao hapa Tanzania.
Katika ziara hiyo, pamoja na kupata taarifa juu ya hatua kubwa ya maendeleo ya Mkoa wa Dodoma. Pia waliweza kujionea kazi kubwa kazi kubwa iliyofanywa ya kuendeleza Makao Makuu ya Nchi na kuimarisha huduma zinazotolewa.
Waheshimiwa Mabalozi walitembelea Hospitali ya Benjamini Mkapa,Mji wa Serikali Mtumba na kujionea ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato ambapo walikiri kuwa kumbe Dodoma ni pa kuhamia leo na sio kesho kama walivyokuwa wakifikiri, na kuahidi kuleta wawekezaji ,watalii, sambamba na kuhamasisha Nchi zao sasa kuona uharaka wa kuhamia Dodoma,kama ilivyokuwa kaulimbiu yetu ya "Ipeleke Dodoma Duniani,Ileta Dunia Dodoma" hakika sasa Dunia itakuja Dodoma.




Nawashukuru sana Waheshimiwa Mabalozi kwa ziara hii ya kimkakati, na ya kuonyesha imani katika uwezo na utayari wa Mkoa wa Dodoma,na ninawakaribisha sana Wawekezaji na Watalii kuja Dodoma na kutumia fursa zilizopo.
Aidha,nawashukuru sana wote tulioshirikiana kuanzia ngazi ya Kitaifa na wananchi wa Dodoma kwa kuendelea kuifanya Dodoma kuwa mahali pa amani na ustawi mkubwa. Mwezi Mei umekuwa wa Furaha.
Dodoma, Fahari ya Watanzania.
Asanteni sana.

**ROSEMARY S. SENYAMULE**
**MKUU WA MKOA WA DODOMA**







**Na.Francisca Mselemu**

## MAONI YA MHARIRI

# SIKUKUU YA WAFANYAKAZI ITUKUMBUSHE JUKUMU LETU LA KUJENGA TAIFA

Sikukuu ya Wafanyakazi, ambayo tumeiadhimisha mwezi huu, ni fursa nzuri ya kutafakari na kukumbuka jukumu muhimu la wafanyakazi katika ujenzi wa Taifa. Wafanyakazi katika ngazi zote na sekta zote, ni nguzo muhimu katika utendaji wa kazi ya Serikali, na katika kuleta maendeleo.

Kazi yetu yenye bidii, ubunifu, na kujitolea ni kiini cha mafanikio yanayowahusu wananchi na ufanikishaji wa malengo ya Kitaifa.

Katika mwezi huu wa sikukuu ya wafanyakazi, tunafurahia kutafakari juhudi kubwa zinazoendelea kufanywa na Serikali ya Awamu ya Sita ili kuleta maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania. Miradi mbalimbali, kuanzia miundombinu, elimu, afya,kilimo na sekta zingine zinaonyesha dhamira thabiti ya Serikali katika kuimarisha uchumi na ustawi wa Wananchi.

Tunaona katika utekelezaji wa miradi hii, kwamba wafanyakazi tuna jukumu kubwa zaidi. Kutokana na upungufu wa rasilimali katika baadhi ya maeneo, wafanyakazi tunahitaji kuonyesha ubunifu na bidii kubwa ili kuleta ufanisi na matokeo yanayotakiwa. Haja ya kuzingatia utendaji kazi wenye tija ni muhimu, hasa katika mazingira magumu au yenye changamoto.

Aidha, wafanyakazi tunapaswa kuendelea kushirikiana na viongozi katika kujenga utaratibu mzuri wa kazi. Hivyo ndivyo Serikali ya Awamu ya Sita inataka. Kujitahidi kutimiza majukumu kwa wakati na kwa ufanisi ni muhimu sana, si tu kwa ufanisi wa miradi bali pia kwa uaminifu wa Serikali mbele ya wananchi.

Sikukuu ya Wafanyakazi inatoa fursa kwa wafanyakazi wote Dodoma na Nchini kote kutoa wajibu wetu kwa Taifa. Kazi ngumu, kujitolea, na kuzingatia utendaji bora, vimekuwa nguzo muhimu za mafanikio. Wafanyakazi tusikate tamaa na tuendelee kuwa chombo cha mabadiliko chanya katika Nchi yetu huku tukizingatia kuwa Serikali, inaendelea kutoa mazingira mazuri ya kazi, mafunzo, na motisha kwetu ili tuweze kuendelea kutoa mchango wetu katika kujenga Tanzania tunayoitaka.

Mshikamano daima na Kazi iendelee.



Na. Hellen M. Minja

# ZIARA YA MABALOZI ILIVYOTIKISA DODOMA



Mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao hapa Tanzania wamehamasishwa kuzishawishi nchi hizo kuwekeza katika Mkoa wa Dodoma kutokana na Mkoa huu kuwa na vigezo vyote muhimu na vinavyojitosheleza kuvutia wageni ikiwemo ardhi ya kutosha kwa ajili ya biashara na uwekezaji inapatikana na uhitaji wake ni mkubwa.

Hayo yamebainishwa na Waziri mwenye dhamana ya Mambo ya nje na Ushirikiano wa Kimataifa Mhe. Balozi Mahmoud Thabiti Kombo alipokua akizungumza na Mabalozi hao kwenye Mkutano na baadae ziara iliyopewa jina la 'Diplomatic Capital City Tour' leo Mei 27, 2025 katika Ukumbi wa Sephil Sepphire Jijini humu.

"Dodoma kuna fursa za biashara na uwekezaji kwa kuwa ina ardhi ya kutosha yenye maji au uwezo wa kuchimba visima, utalii, Mahoteli na uhitaji wake ni mkubwa sana. Maeneo yanayoonekana kuwa mbali na mji, muda si mrefu hayataonekana kuwa mbali kwa sababu mahitaji ya makazi na Mahoteli ni makubwa mno hivyo changamkieni fursa hii".

Aidha, Naibu Waziri wa TAMISEMI Mhe. Zainab Katimba amesema Serikali katika kipindi hiki cha miaka minne imewekeza zaidi ya shilingi Trilioni 5.1 kwenye uboreshaji wa elimu ambapo takribani shule za Msingi 1,399 na shule za sekondari 1,044 zimejengwa sambamba na ujenzi wa Mabweni, Maabara pamoja na nyumba za walimu.

Hata hivyo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma amezungumzia miradi ya kimkakati inayotekelezwa Mkoani hapa ambayo inaufanya kuwa na hadhi ya Makao Makuu ya nchi na kuwa chachu ya kuvutia wawekezaji kutoka nje ya nchi.

"Serikali imewekeza miradi mikubwa ikiwemo ujenzi wa Mji wa Serikali Mtumba, ujenzi wa Reli ya mwendo kasi (SGR), ujenzi wa barabara ya mzunguko wan je, Kiwanja cha ndege cha Kimataifa Msalato, miundombinu ya umwagiliaji, kituo cha kupozea umeme kutoka Bwawa la Mwalimu Nyerere ambapo miradi yote imegharimu zaidi ya shilingi Trilioni 10".

Akizungumza baada ya hafla hiyo, Balozi wa China nchini Mhe. Dr. Lu Youqing, amesema nchi yake inaunga mkono maendeleo ya Tanzania na ameshawishi makampuni ya nchini mwake kutembelea Dodoma na kuleta shughuli zao za kibiashara hapa ili kupata maendeleo ya kibiashara pamoja.

Naye, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma Dkt. Fredrick Sagamiko ametumia wasaa huo kuelezea juu ya mradi unaotarajiwa kutekelezwa Hombolo kwa kuufanya kuwa Mji wa Kidiplomasia kutokana na uwepo wa Ziwa Hombolo ambalo lipo umbali wa Km 70 kutoka Dodoma Mjini na eneo hilo ni la kimkakati kwani lipo karibu na Mji wa Serikali, eneo la Mabalozi pia kiwanja cha ndege cha Msalato.

Sanjari na Mkutano huo, Mabalozi hao walipata fursa ya kutembelea miradi kadhaa ya kimkakati kwa kuanzia kwenye huduma za afya ambapo walitembelea Hospitali ya Kanda ya Benjamin Mkapa na kujionea huduma za kisasa zinazotolewa, walitembelea ujenzi wa Mji wa Serikali Mtumba na mwisho walitembelea mradi wa Kiwanja cha Ndege Msalato.

'Capital City Diplomatic Tour', imeandaliwa kwa kutambua mchango wa Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye amejenga mahusiano mazuri na nchi zote Duniani,hali inayowafanya wafurahie kuja Tanzania, na haya yote wamekua wakiyafanya katika nchi mbalimbali hivyo sasa ni zamu ya Dodoma.

Kaulimbiu: "Dodoma ipo Tayari kwa Ajili yenu (Dodoma We are Ready For You)"

# DODOMA YADHAMIRIA KUJIKITA KWENYE KILIMO CHA MATUFAA (APPLES) KUINUA UCHUMI

Na. Hellen M. Minja,



Mkoa wa Dodoma umedhamiria kujikita kwenye ukuzaji wa uchumi kupitia kilimo cha matunda aina ya Tufaa (Apple). Hii ni kufuatia kauli ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule aliyoitoa alipotembelea Shamba Darasa lililopo eneo la Chinangali II Wilaya ya Chamwino linalozalisha matunda hayo Mkoani hapa kwa lengo la kujifunza uzalishaji wake.

Akiwa shambani hapo, Mhe. Senyamule alipata ufahamu wa namna tunda hilo linavyozalishwa na kutoa rai kwa wanadodoma kujikita kwenye uzalishaji wa tunda hilo adhimu Nchini ambalo hupatikana kwa wingi kwa kuagizwa nje ya nchi hususani nchini Afrika ya Kusini.

“Sisi kwa sababu zao hili halijalimwa katika Mikoa mingi kama zao la kimkakati, tukasema ili kupunguza ushindani na mikoa mingi, tuje na zao la Apple ambalo kwa sasa litakua linapatikana Dodoma. Majaribio ni haya tumeyaona ambayo hili hapa kwetu ni shamba darasa la Mkulima binafsi ambaye alianza kulima mwaka jana na ametusimulia jinsi alivyoona matokeo makubwa.”



Aidha, Mhe. Senyamule amezungumzia soko la Matufaha ambalo ni kubwa kutokana na wingi wake unaoingizwa kutoka nje ya nchi hivyo, endapo kama Mkoa wa Dodoma utafanya kilimo hicho, soko la kutosha linapatikana.

“Apple uzuri wake lina sifa nyingi, bado lina soko kubwa la ndani kwa sababu mengi tunaingiza kutoka nje ya nchi kwa sababu nchi yetu haijaweza kulima ya kujitosheleza, lakini lina soko kubwa la ndani, kama tukilima ndani ya nchi na ikashuka kidogo, bado itakua ni bei nzuri ya kumfurahisha Mkulima.” Ameongeza Mhe. Senyamule.

Aidha, Mkurugenzi wa ‘Mtimbi’s Farm’ Bw. David Mtimbi Mwaka ambaye shamba lake linatumika kama darasa kujifunza kuhusu kilimo cha Matufaha, ameelezea namna alivyoguswa kuanzisha kilimo hicho.

“Niliweka kama majaribio miche 100 nikawa navutiwa kuona kama itakua kama ‘apple’ ya South Afrika au itakua kama tulizozizoea za Tanga na sehemu nyingine? Baada ya kupanda niliambiwa zitaanza kuzaa baada ya miaka miwili na nusu, ili ikue vizuri unatakiwa kumwagilia na zilianza kuzaa katika kipindi cha mwaka mmoja hivyo inawezekana na zina ladha nzuri.”

Mbali na kutembelea shamba darasa hilo, Mhe. Senyamule alipata fursa ya kutembelea mradi wa kilimo cha umwagiliaji unaotekelezwa na kikundi cha Wanyausi Manchali ‘A’ kilichoanzishwa 19/12/2023 ikiwa ni mpango wa Serikali kupitia Wizara ya Kilimo (BBT) kuwachimbia visima na kuweka miundombinu ya umwagiliaji kwa wakulima wadogo.

Mashamba hayo yamewezeshwa kwa kuchimbiwa kisima chenye urefu wa mita 160 kikiwa na uwezo wa kuhudumia mashamba 150 huku Bwawa likiwa na uwezo wa kubeba maji ujazo wa lita 850,000. Mradi huo umesaidia kuboresha lishe kwa wakulima na jamii inayozunguka eneo hilo, kuongeza maarifa kwa kutumika kama ‘shamba darasa’ pamoja na kuimarisha kipato cha Wakulima.

# DHAMIRA YA MHE. RAIS, WATANZANIA KUPATA HUDUMA YATIMIA KWA MKOA WA DODOMA

Na. Hellen M. Minja


Dhamira ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuona Viongozi wa Wilaya wanawatumikia Watanzania kwa dhati, bila vikwazo, imetimia leo Mei 21, 2025 kwa Mkoa wa Dodoma kukamilisha magari ya Wakuu wa Wilaya zote saba, ambapo Mkuu wa Wilaya ya Dodoma amekabidhiwa gari mpya.




Makabidhiano hayo yamefanyika nje ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma na baada ya makabidhiano hayo, Mkuu wa Mkoa Mhe. Rosemary Senyamule akapata wasaa wa kuzungumza machache juu ya dhamira ya Mhe. Rais.

"Wakuu wa Wilaya zote saba za Mkoa wa Dodoma wamekamilika kupata magari ndani ya huu mwaka mmoja wa fedha (2024/2025). Tunajua jambo hili ni dhamira yake ya dhati kuona Viongozi hawa wanawatumikia Watanzania kwa dhati kabisa, bila kikwazo cha kuwafikia vijijini, milimani, mabondeni, magari haya yanafika".

Kwa upande wake Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma Bw. Kaspar K. Mmuya, amemtaka Dereva wa gari hilo kulitunza na kufuata sheria, kanuni na taratibu za usalama barabarani, kwa kuzingatia mafunzo yaliyotolewa hivi karibuni kwa madereva wa magari ya Serikali.



"Haya ambayo utakwenda kuyafanya ni matokeo ya mafunzo haya, nakukumbusha tu kulinda usalama wako na mali ya Umma, na usiwe mfano bora wa kuvunja sheria za barabarani. Matumizi ya ving'ora na taa za vimulimuli yamekatazwa, kwa hiyo ukisimamishwa na Polisi, simama, msikilize kisha songa mbele, usimkatalie Polisi kutimiza wajibu wake hata kama hakuna kosa".

Mnamo Mei 17, 2025, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma SACP George Katabazi, aliitisha kikao maalumu kwa Madereva wa Magari ya Serikali kilichokwenda sambamba na mafunzo yaliyotolewa juu ya kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za usalama barabarani kutokana na malalamiko yanayoelekezwa kwa Madereva hao juu ya uvunjifu wa sheria za barabarani.









## KAMPUNI YA 'CAVO' YA CHINA YATAFUTA FURSA ZA UWEKEZAJI DODOMA

Na. Hellen M. Minja,

Wawakilishi kutoka Kampuni ya Kimataifa ya CAVO ya nchini China, wamefika ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule iliyopo Jengo la Mkapa Jijini Dodoma, Mei 05, 2025 kwa ajili ya mazungumzo yaliyolenga kutafuta fursa za uwekezaji Mkoani hapa hasa katika kilimo cha Alizeti.

Waliofika Ofisini hapo ni Bi. Jessicattan na Bw. Xu Shao ambapo mbali na kilimo, wamejinasibu kuwa Kampuni yao inajihusisha na utengenezaji wa maeneo ya vivutio kwa ajili ya Utalii na biashara hivyo, Mhe. Senyamule amewakaribisha na kusema kuwa bado Mkoa unahitaji wawekezaji wa kutosha kutokana na hadhi yake ya Makao Makuu ya Nchi.

# WATUMISHI HODARI 2025 KUTOKA OFISI YA MKUU WA MKOA WA DODOMA WAPONGEZWA

Na. Hellen M. Minja



Watumishi Hodari kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, wamepongezwa kwa kujitoa na kujituma kufanikisha shughuli mbalimbali za Mkoa huu hali iliyosababisha wachaguliwe kuwawakilisha wengine kwenye zawadi za wafanyakazi hodari wakati wa sherehe za Mei Mosi 2025 zilizofanyika Kitaifa Mkoani Singida.

Pongezi hizo zimetolewa Mei 09, 2025 na Mkuu wa Mkoa huyo Mhe. Rosemary Senyamule alipozungumza kwa njia ya simu na Watumishi hao kwenye hafla fupi ya chakula cha pamoja iliyoambatana na kuwapongeza Watumishi Hodari akiwemo Mtumishi Hodari wa jumla Mhandisi David Chitemo.

"Tumezifanya shughuli zile kwa ushirikiano mkubwa na najua watumishi walikua tayari. Pia nawapongeza wale wenzetu waliotuwakilisha kwa kupata zawadi za kuwa wafanyakazi hodari,ambapo pamoja na zawadi zile, niliagiza leo tufanye shughuli maalum ya kuwapongeza na kuwakabidhi zawadi zetu." Mhe. Senyamule.

Aidha, Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma Bw. Kaspar K. Mmuya ametumia jukwaa hilo kuwahimiza Watumishi wake kuwekeza kwenye kilimo cha matunda ya Matufaha 'Apples' ambacho kinaonekana kitafanya vizuri katika Mkoa wa Dodoma na soko lake ni kubwa.

"Uzuri wa 'apples', baada ya kuvuna inaanza tena, yaani inazaa 'continuously'. Mkuu wa Mkoa alikwenda akapiga picha, tumeona 'apples' ambazo zilivunwa na ukiziona huwezi kuamini kama ni za Dodoma, unaweza kufikiri zimetoka South Afrika. Sasa tunakwenda kuhamasisha hili jambo na tunasikia zinapatikana Iringa, na mche ni shilingi 12,000 tu".

Akitaja vigezo na sifa za kuchaguliwa kuwa Mfanyakazi hodari wa mwaka, Katibu Tawala Msaidizi Seksheni ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali watu Mkoa wa Dodoma Bi. Coletha Kiwale;

"Baadhi ya vigezo vya kupata Mfanyakazi hodari ni yule ambaye sio malalamishi, anayeweza kupokea ushauri kutoka kwa Watumishi wengine, Mfanyakazi ambaye ni mbunifu lakini ambaye pia anatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu lakini pia anaweza kupokea ushauri kutoka kwa Watumishi wengine."

Watumishi Hodari 2025 waliopongezwa ni Mhandisi David Chitemo (Seksheni ya Uchumi na Uzalishaji), Bi. Grace Moshi (Kitengo cha TEHAMA), Bi. Vaileth Nanyaro (Seksheni ya Usimamizi, Ufuatiliaji na Ukaguzi), Bw. Jacob Mang'ombe (Seksheni ya Utumishi), Bw. Moses Kawage (Ukaguzi wa ndani), Bi. Salma Kilili (Seksheni ya Elimu), Dr. Peres Lukango (Seksheni ya Afya) na Mhandisi Ismail Kilima (Seksheni ya Miundombinu).

# WAZAZI WASISITIZWA KUPELEKA WATOTO SHULE KUFUATIA KUIMARIKA KWA MIUNDOMBINU YA ELIMU

Na. Hellen M. Minja



Msisitizo unazidi kutolewa kwa wazazi wa Mkoa wa Dodoma juu ya umuhimu wa kuwapekeka watoto wao shule kwani Serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imewekeza fedha nyingi kwenye ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu katika Mkoa huu.

Hayo yamebainishwa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule alipokua akizungumza na wakazi wa Kata ya Paranga, Halmashauri ya Wilaya ya Chemba Mei 08, 2025 katika Mkutano wa hadhara mara baada ya kutembelea na kukagua miundombinu ya shule na mabweni katika baadhi ya shule zilizopo Wilayani humo.

"Chemba ni moja ya Wilaya ambayo inatuvuta nyuma kwenye matokeo ya Mitihani ya mwisho. Kwa hiyo, kwenye elimu tusifanye mchezo, lindaneni wenyewe, hakikisha mtoto anakwenda shule, manufaa yake mtayaona, elimu inalipa wala haichelewi". Amesisitiza Mhe. Senyamule.

Licha ya suala la elimu, Mhe. Senyamule amewahimiza wakati hao kuhusu suala la uchumi kupitia kilimo cha matunda hususan Matufaha (Apples) kwani utafiti umefanyika na kuonekana yanafanya vizuri katika ardhi ya Dodoma pia yana soko kubwa hivyo, matamanio ya Serikali ya Mkoa ni kuona mabadiliko ya uchumi kwa wananchi wake.

Akizungumza katika hadhara hiyo kabla ya kumkaribisha Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya ya Chemba Mhe. Halima Okash, amesema Serikali imefanya kazi kubwa kwa kuwekeza fedha nyingi katika Kata hiyo ambapo zaidi ya shilingi Bilioni 11.5 kwenye miradi ya Maji, Milioni 60 kwa ajili ya Maabara mbili, madarasa yenye thamani ya zaidi ya Milioni 360.

Miradi iliyotembelewa na Mkuu wa Mkoa ni pamoja na ujenzi wa shule ya wavulana ya Kanda ambayo inagharimu kiasi cha shilingi Bilioni 4.6 kupitia mpango wa kuboresha elimu (SEQUIP) na inatarajiwa kukamilika June 2025 ambapo mradi huo unalenga kutoa elimu kwa wanafunzi 960 wa kanda ya kati kwa ngazi ya O-level na A-level .

Ujenzi wa Bweni katika shule ya Sekondari Mrijo unaotekelezwa kwa fedha za Serikali kuu kupitia EP4R, mapato ya ndani na nguvu za wananchi ambapo unagharimu kiasi cha shilingi Milioni 214.4, Mradi wa ujenzi wa Hosteli katika shule ya Sekondari Jangalo unaogharimu kiasi cha Shilingi Milioni 144.4

Lengo la ujenzi wa Mabweni na Hosteli katika shule hizo ni kupatikana kwa elimu bora kwa wanafunzi wa Kata hizo, kupunguza changamoto za wanafunzi kutembea umbali mrefu kufika shuleni, kutoa nafasi ya elimu bora pamoja na kupunguza adha na madhila wanayopata hasa wasichana kutoka kwa vijana wa mtaani maarufu kama 'maronjoo'.



# MTUMISHI HODARI WA JUMLA 2025 OFISI YA MKUU WA MKOA WA DODOMA, APONGEZWA KIPEKEE

Na. Hellen M. Minja

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma imempongeza kipekee Mtumishi Hodari wa jumla 2025 wa Taasisi yake ambaye ni Mhandisi David Isaya Chitemo anayetumikia Seksheni ya Uchumi na Uzalishaji, ambapo amepongezwa kwa kujituma usiku na mchana kutimiza majukumu yake hali iliyofanya aonekane kuwa anastahili pongezi.

Mhandisi Chitemo ametajwa kuwa na sifa za ziada katika utendaji wake,sifa ambazo zimempa kukidhi vigezo vya kuwa mtumishi hodari wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma. Miongoni mwa sifa hizo ni kutimiza majukumu anayopangiwa kwa wakati,kufanya kazi kwa kujituma bila kujali uchache wa vitendea kazi wala muda anaofanya kazi.

Katika kumpa motisha Mfanyakazi huyo hodari wa Taasisi, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma imetoa zawadi kadhaa ikiwemo shilingi Milioni Mbili, fedha taslimu za Kitanzania, barua ya pongezi kutoka kwenye Uongozi wa Taasisi pamoja na kutengenezewa picha kubwa ya ukutani itakayowekwa eneo la kusaini mahudhurio mwaka mzima, ili kila Mtumishi aweze kumuona anapoingia ama kutoka ofisini.



# SOKO LA MACHINGA DODOMA KUANZISHA DAWATI LA JINSIA KUPAMBANA NA UPOTEVU WA HAKI

Na. Hellen Minja

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma ameelekezwa kuhakikisha kuwa soko la wafanyabiashara wadogo wadogo Jijini Dodoma maarufu kama 'Machinga Complex' linakuwa na dawati la jinsia ndani ya kituo kidogo cha Polisi kilichopo sokoni hapo ili kukabiliana na vitendo vya upotevu wa haki ya kijinsia.

Maelekezo hayo yametolewa Mei 12, 2025 na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule alipokua akizindua rasmi Umoja wa Wanawake Machinga Dodoma (UWAMADO) katika hafla iliyofanyika kwenye viwanja vya soko hilo Jijini Dodoma.

"Kama hapa kuna viashiria vya kupoteza haki ya kijinsia, hakikisheni leo tarehe 12, 05 hadi tarehe 30, Dawati la kijinsia liwe limeanzishwa hapa ili muweze kupata haki sawa. Nchi yetu haitaki kupendelea mtu mmoja, wanaume au wanawake, inataka wote wapate haki sawa, kituo cha Polisi tayari kipo hivyo, unao mwanzo wa kuanzia ili hili liweze kutokea".

Akizungumza na wanawake hao pamoja na hadhira iliyojitokeza kushuhudia uzinduzi huo, Mbunge wa Dodoma Mjini na Waziri wa Nishati Mhe. Anthony Mavunde amesema Jiji la Dodoma limetenga shilingi Bilioni 7 kwa ajili ya kutoa mikopo kwa akina Mama, vijana na watu wenye ulemavu hivyo ameyataka makundi hayo kuchangamkia fedha hizo.

Nae, Meneja Msaidizi wa Soko la Machinga Bw. Mbwana Kasonta, amemshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwajengea soko hilo ambalo limepunguza adha ya kupigwa na jua pamoja na mvua mitaani hivyo limeongeza wateja wa kudumu sambamba na kuliweka Jiji katika hali ya usafi.

Awali, akisoma risala ya Umoja huo, Katibu wake Bi. Mariam Kajembe amesema, Umoja wao una ndoto ya kuanzisha SACCOS ili kupambana na ukosefu wa mitaji rafiki kwa ajili ya kufanyia biashara kwani wamekua wahanga wa kukosa mitaji ya kuendeshea biashara ambapo kuunga mkono hilo, zimetolewa shilingi Milioni 4 kuanzisha SACCOS hiyo.





# WAKAZI WA BUSI-KONDOA WATAHADHARISHWA JUU YA UTUNZAJI WA VYANZO VYA MAJI

Na. Hellen Minja

Wananchi wa Kata ya Busi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa wametakiwa kuchukua tahadhari juu ya utunzaji wa vyanzo vya maji, kwani kwa sasa maji yanazidi kupungua kutokana na ongezeko la watu kila uchao lakini maji hayaongezeki.

Tahadhari hiyo imetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule Mei 13, 2025 alipokua akizungumza na wananchi hao wakati wa Mkutano wa hadhara uliofanyika katika viwanja vya Mahakama ya mwanzo ya Kata hiyo baada ya kutolewa kero ya ukosefu wa maji.

"Tunapoelekea maji yatazidi kupungua, na wenzetu wanatuambia vita kubwa Duniani itakayokuja ni kugombania maji.Kama tusipochukua tahadhari leo kuanza kutumia maji kwa vipimo, kutumia maji kwa tahadhari kutunza vyanzo vya maji ili yasipungue kwa sababu watu tunaongezeka kila siku lakini maji ni yaleyale. Hili jambo lipo mikononi mwenu".




Aidha, Meneja RUWASA Wilaya ya Kondoa Mhandisi Loini Merinyo, amesema changamoto kubwa inayoikabili Kata hiyo ni wizi wa miundombinu ya maji hasa koki za kufungulia matenki ya kuhifadhia maji ambazo zimekua zikiibiwa kila zinapowekwa hali inayosababisha upotevu wa maji kwa kiasi kikubwa.

Awali, Mkuu wa Mkoa alitembelea mradi wa ujenzi wa nyumba nne za walimu katika shule ya msingi Foe iliyopo katika Kata ya Kalamba Halmashauri ya Kondoa ikiwa na jumla ya wananfunzi 402 wakiwemo wavulana 199 na wasichana 203 huku ikiwa na walimu watano walioajiriwa na wawili wakujitolea.

Mradi huo wenye thamani ya shilingi milioni 201.9 kutoka Mamlaka ya Elimu Tanzania na upo kwenye hatua za umaliziaji ambapo unatarajiwa kumaliza changamoto ya upungufu wa nyumba za walimu shuleni hapo hali itakayosaidia kuimarisha utoaji wa huduma ya elimu kwa wanafunzi wa Kata hiyo.

Akiwa shuleni hapo, Mhe. Senyamule alipata fursa ya kuzungumza na Wazazi pamoja na Wanafunzi wa shule hiyo amesema kuwa uongozi wa Mkoa na Wilaya hiyo utahakikisha unaangalia namna ya kushughulikia mradi huo ukamilike haraka ili Walimu wafaidike kama ambavyo Mhe. Rais alikusudia.


OFISI YA MKUU WA
MKOA WA DODOMA
MHE. ROSEMARY SENYAMULE
MKUU WA MKOA WA DODOMA
KERO YAKO,
WAJIBU WANGU



Na. Hellen M. Minja

# RC SENYAMULE AZUNGUMZA NA MAKUNDI MBALIMBALI MKOANI MWAKE

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule amekutana na viongozi wa makundi mbalimbali yanayopatikana katika Mkoa huu leo Mei 15, 2025 katika ukumbi wa ofisi yake iliyopo jengo la Mkapa Jijini Dodoma. Lengo la makutano hayo ni kuzungumzia mambo tofauti tofauti yanayohusiana na Mkoa ikiwa ni pamoja na kuwasisitiza kuhakiki na kuhuisha majina yao kwenye Daftari la Kudumu la Mpiga kura zoezi lililokwisha anza ili wawe na sifa za kushiriki Uchaguzi Mkuu mwaka huu 2025.



Aidha, Mhe. Senyamule alizungumzia vipaumbele vya Mkoa ambavyo ni kilimo cha matunda hasa 'Apples', Utalii, Madini, Mji wa kilojistiki, Viwanda na Biashara pamoja na kujiandaa na maandalizi ya ziara ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan iliyopewa jina la 'Samia Day' anayotarajia kuifanya Mkoani hapa Mwezi Juni, 2025.

# WANAFUNZI WA KIDATO CHA SITA WAASWA SAFARI YA ELIMU BADO NI NDEFU

Na. Hellen M. Minja



Wanafunzi wameaswa kuwa safari ya kutafuta elimu ni ndefu na yenye kuhitaji vipawa na malengo mahsusi ili kuweza kupata mafanikio na maendeleo katika Taifa. Hayo yamesemwa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule wakati wa mahafali ya kuwaaga wanafunzi wa kidato cha sita wa shule ya Sekondari Maria de Mattias.

Katika Mhafali hayo ya 10 yaliyofanyika leo Mei 17, 2025, kwenye ukumbi wa shule hiyo iliyopo Kisasa Jijini Dodoma, Mhe. Senyamule ametoa hotuba yake iliyogusa vipengele kadhaa vyenye kuwausia wanafunzi hao juu ya maisha nje ya shule ambapo aliwekea mkazo suala la elimu.

"Safari iliyopo mbele bado ni ndefu na kubwa, inahitaji vipawa, watu wenye malengo, wachapakazi, wenye bidii kubwa, waaminifu na kwa sababu ni watoto wa kike na kiume, inahitaji watu wanaojitambua na wanaojitunza. Kujitunza ni wajibu wa kila mmoja, lakini inahitaji watu majasiri na wenye ubunifu wa kufanya mambo."

Hata hivyo, mwakilishi wa Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma ambaye ni Afisa Elimu Taaluma Mwl. Justin Machela, amezungumza na wazazi wa wahitimu hao na kuwasisitiza juu ya malezi mema kwa watoto wao ambao bado wanahitaji uangalizi wa karibu wa wazazi kwani sasa wanatoka mikononi mwa Walimu na wanakwenda kuwa chini ya uangalizi wao.




Vilevile, Mkuu wa Shule hiyo Sister Theresia Mkuyi, amewataka Wahitimu kuendelea kuwa na nidhamu, maadili mema na kutumia maarifa waliyopata shuleni hapo kwa manufaa yao binafsi na jamii kwa ujumla, huku wakiwa waangalifu kwenye matumizi ya teknolojia na kuwa Mabalozi wazuri wa shule hiyo.

Shule ya Sekondari Maria de Mattias, ilianzishwa mwaka 2010 chini ya uongozi wa Shirika la Masista wanao abudu Damu ya Kristo ikiwa na wanafunzi 90 wa kidato cha kwanza kwa lengo la kuwalea Wasichana kielimu, kimwili, kiroho na kimaadili. Kwa sasa, shule hiyo ina jumla ya wanafunzi 535 kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita.

# VIVUTIO VYA UTALII NA AINA ZA UTALII DODOMA



## IDODOMYA

Mahali ambapo tembo alizama na kutengeneza asili ya jina Dodoma. Kivutio hiki kinapatikana katika eneo la Kikuyu linalopatikana umbali wa kilomita 3 kutoka katikati ya Jiji.



## MPWAPWA

Nyumba aliyofikia Mwl. Nyerere

Nyumba hii ndipo ambapo Mwl. Julius K. Nyerere alikaribishwa na wazee wa Mpwapwa kwa mara ya kwanza na ndipo alipokuwa akifikia mara tu baada ya kufika katika eneo hilo wakati wa kudai uhuru wa Tanganyika. Nyumba hii ipo katika Mtaa/ Barabara ya Kikombo.



## KONGWA

**KABURI LA CHIFU/ MTAWALA ALIYEZIKWA AKIWA AMEKA**

Kaburi hili linalopatkana katika Wilaya ya Kongwa, ndipo ambapo alizikwa Chifu wa eneo hilo ambaye alifahamika kwa jina la Mtemi Mdabuko. Mtemi huyu aliheshimika sana na watawaliwa wake kwani alikuwa amejaaliwa uwezo wa kufanya miujiza mikubwa katika eneo hilo kama vile kuleta mvua katika kipindi ambacho kulikuwa hakuna mvua ilhali inahitajika kwa shughuli mbalimbali ikiwemo kilimo.

# MADEREVA WA SERIKALI WATAKIWA KUZINGATIA SHERIA ZA USALAMA BARABARANI

Na. Hellen M. Minja

Madereva wa magari ya Serikali wametakiwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa kwa ajili ya usalama barabarani pindi wanapokuwa wakiendesha magari hayo.

Hayo yamebainishwa Mei 17, 2025 na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma SACP George Katabazi wakati akizungumza na madereva hao kwenye kikao maalumu alichokiitisha katika ukumbi wa PGA Jijini Dodoma kilicholenga kuzungumza nao juu ya utii wa sheria za usalama barabarani kwani baadhi yao wamekuwa wakilalamikiwa kukiuka sheria hizo.

"Kikubwa ni kuwataka Madereva wa Serikali kuzingatia sheria na taratibu zinazohusiana na usalama barabarani. Tunawakaumbusha, tunawaelimisha kuhusiana na sheria hizo, taratibu na kanuni lakini pia kuwaonya baadhi yenu ambao hawazingatii sheria za usalama barabarani. Tunawakemea wale ambao kwa makusudi wanavunja sheria hizo".




Aidha, Kamanda Katabazi ameongeza kuwa wana andaa utaratibu ambao utahusisha kuundwa makundi sogozi yatakayohusisha Viongozi wa Madereva wa Serikali katika kila Mkoa pamoja wasimamizi ambao ni Maafisa usalama barabarani wa Mikoa husika.

Akizungumza baada ya kikao hicho, Mwenyekiti wa chama cha Madereva wa Serikali Bw. Issa Kisebengo amesema kuwa elimu waliyoipata kwenye kikao hicho imewasaidia kutambua majukumu na wajibu wao kwenye Utumishi wa Umma na kutoa wito kwa madereva wenzake.



"Sisi ni vioo kwa madereva wengine lakini pia tunabeba Watumishi wa Serikali, na kuna watumiaji wengine wa barabara,wote hao wanatutegemea sisi kwa usalama wao hivyo, mafunzo tuliyoyapata hapa, tusiyaache hapa hapa, tuyabebe, tuyatunze na twende tukayafanyie kazi".

Licha ya kukumbushwa sheria, kanuni na taratibu za usalama barabarani, kikao hicho pia kiliambatana na mafunzo mbalimbali yaliyotolewa kwa madereva hao ili kuendelea kuwakumbusha kuhusu kuzingatia sheria hizo kwani kuwa madereva wa magari ya Serikali si kigezo cha kuvunja sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.

# CMSR WAMALIZA MRADI WA UBORESHAJI HUDUMA ZA AFYA YA UZAZI NA MTOTO JIJINI DODOMA

Na. Hellen M. Minja.



Wadau wa Afya kutoka Shirika la 'Community Mobilization of Reciprocal Development' (CMSR) kutoka Italia linalofadhili mradi wa uboreshaji huduma za afya ya Uzazi na Mtoto katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma, leo Mei 19, 2025 wamemtembelea Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma Bw. Kaspar K. Mmuya Ofisini kwake Jijini Dodoma kwa lengo la kumuaga kwani wamefikia tamati ya mradi huo Mkoani hapa.

Mradi huo uliokua ukitekelezwa kwa kipindi cha miaka miwili, unafikia ukomo wake mwisho wa mwezi Juni ambapo katika kipindi hicho matokeo makubwa yameonekana katika vituo vilivyokua chini ya ufadhili kwani lengo kubwa ni kuboresha huduma za Mama na Mtoto na kukomesha vifo vitokanavyo na uzazi na watoto.

Aidha, Bw. Mmuya, amewashukuru wadau hao kwa Mradi ambao unanufaisha Mama na Mtoto kwenye jamii huku akiwaomba kutanua wigo hapa Makao Makuu ya Nchi.



"Mradi huu unaboresha familia na unahitajika zaidi maeneo ya Miji kama Bahi, Chamwino, Chemba na mengineyo. Kama mnaweza kuongeza wigo kidogo tutakua na furaha sana kwa sababu nahitaji uwepo wenu, msiende mbali na Makao Makuu wala Tanzania, tunahitaji huduma bora za afya kila eneo ili kufikia lengo".

Shirika hilo limetekeleza mradi huo kwenye vituo vya afya vinne ambavyo ni Hospitali ya St. Gemma, Kituo cha Afya Mkonze, Kituo cha Afya Hombolo na kituo cha afya Makole. Wadau hao wamewajengea uwezo watoa huduma wa Mama na Mtoto lakini pia wamewezesha ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa kwa ajili ya huduma hizo.

Na. Hellen M. Minja

# RAS MMUYA ATEMBELEA MAONESHO KUELEKEA KILELE CHA SIKU YA NYUKI DUNIANI

Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma Bw. Kaspar K. Mmuya leo Mei 19, 2025 ametembelea mabanda ya maonesho ya Nyuki na bidhaa za Nyuki yanayofanyika kwenye viwanja vya Bustani ya mapumziko Chinangali (Chinangali Park) Jijini Dodoma.

Maonesho hayo yaliyoanza Mei 17 yanatarajiwa kutamatika siku ya Jumanne Mei 20, ambayo ndio Kilele cha Maadhimisho ya siku ya Nyuki Duniani yanayolenga kutambua mchango wa mdudu nyuki katika usalama na uhifadhi wa chakula.

Akiwa viwanjani hapo, Bw. Mmuya amepata fursa ya kutembelea mabanda kadhaa yanayotengeneza bidhaa zinazotokana na nyuki pamoja na kupata elimu juu ya mambo mbalimbali yayoweza kufanyika kwa kutumia mdudu huyo, sambamba na kutembelea wanyama pori ambao nao wamekua kivutio kwenye maonesho hayo.

Mgeni rasmi katika kilele cha Maadhimisho ya mwaka huu anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (MB), ambapo kaulimbiu ni “Nyuki kwa Uhai na Uchumi Imara, Tuwahifadhi”.








Na. Hellen M. Minja

# TANZANIA NCHI YA KWANZA AFRIKA MASHARIKI KUZALISHA TANI 34,000 ZA ASALI



Imeelezwa kuwa Tanzania inazalisha asali kiasi cha tani 34,000 na kuiweka katika ramani ya dunia kuwa nchi ya kwanza Afrika Mashariki kwa uzalishaji huo lakini pia inashika nafasi ya pili Barani Afrika.

Hayo yamebainishwa na Waziri Mkuu wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (Mb) wakati akihutubia hadhara iliyojitokeza kwenye kilele cha maadhimisho ya siku ya nyuki Duniani kilichofanyika leo Mei 20, 2025 kwenye viwanja vya Bustani ya Mapumziko Chinangali Jijini Dodoma.

"Kwa sasa Tanzania inazalisha tani 34,000 za asali. Kiwango hiki kinaiweka Tanzania katika ramani ya Dunia kwa kuwa nchi ya kwanza kwa uzalishaji wa asali kwa nchi za Afrika Mashariki, lakini pia katika Bara la Afrika, Tanzania ni nchi ya pili, kwenye hesabu ya Duniani, tumeshika nafasi ya 14 kati ya nchi zote".

Kadhalika, Waziri mwenye dhamana ya Maliasili na Utalii Mhe. Balozi Pindi Channa, amesema kuwa lengo la maadhimisho hayo ni kutambua mchango wa mdudu nyuki na nafasi ya Tanzania katika maendeleo ya ufugaji nyuki Duniani hivyo wamefanya midahalo, semina na kutoa elimu kwa jamii juu ya uelewa wa siku hiyo.

Hata hivyo, Waziri Mkuu Mstaafu na mdau muhimu wa nyuki kwa Mkoa wa Dodoma Mhe. Mizengo Pinda ametoa ushauri kwa vijana kujihusisha na ufugaji nyuki ili kuinua kipato kupitia mazao yake pamoja na kuiusia jamii kuendelea kumuona mdudu huyo kama rafiki kutokana na msaada wake katika utunzaji wa misitu yetu.



Naye, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule amesema Mkoa wake unaendelea kuhamasika katika ufugaji wa Nyuki kwa maslahi mapana ya Mkoa na Taifa kwa ujumla.

"Mkoa wa Dodoma umekua ni kati ya Mikoa inayohamasisha ufugaji wa nyuki, na inao wafugaji wa nyuki, lakini pia tunafurahi kuwa tuna viwanda vitatu ambavyo vinaendelea kuchakata mazao ya nyuki na kuuza. Na tunamshukuru Mhe. Mizengo Pinda kwani shamba lake limekua 'shamba darasa' na kufanya Wanadodoma kuwa wafugaji wa Nyuki".

Maadhimisho ya siku ya nyuki duniani ni utekelezaji wa Azimio la Baraza la Umoja wa Mataifa la tarehe 20 Desemba, 2017 ambalo lililenga kutambua mchango wa mdudu nyuki katika usalama na uhifadhi wa chakula na kauli mbiu ya maadhimisho ya mwaka huu 2025 ni "Nyuki kwa Uhai na Uchumi Imara, Tuwahifadhi".

# DODOMA YATAJWA KUFANYA VIZURI KWENYE KILIMO CHA MBOGAMBOGA NA MATUNDA.

Na. Hellen M. Minja,




Mkoa wa Dodoma unatajwa kufanya vizuri kwenye kilimo cha mbogamboga na matunda endapo utapata wawekezaji wenye nia ya dhati, kwani soko la uhakika linapatikana,na lengo ni kuondokana na umasikini kupitia kilimo hicho.

Hayo yamebainishwa na Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma Bw. Kaspar K. Mmuya wakati wa zoezi la makabidhiano ya mbolea kiasi cha tani moja iliyotolewa na kiwanda cha mbolea cha Itracom kilichopo Nala Jijini Dodoma kwa Shirika lisilo la Kiserikali la CDIS linalosimamia mradi wa kilimo wenye lengo la kutengeneza fursa za ajira kwa vijana.

“Kilimo cha ‘hot-culture’ kinawezekana sehemu yoyote, nimefuatilia kuna mambo mawili, aina ya mbegu na magonjwa, nasisitiza hilo eneo lifanyiwe kazi. Mkuu wa Mkoa kwenye eneo la kilimo yupo ‘serious’ sana, na sasa hivi anaongoza kwa maneno na vitendo kwa kupanda miti ya matunda Mkoa wote huu wa Dodoma hasa Parachichi. Dodoma kuna soko kubwa kwani Watumishi wa Serikali wapo Dodoma, Wizara zipo hapa, Taasisi na Wafanyabiashara wakubwa wote wapo hapa, fedha zinatokea Dodoma .Njooni muwekeze Dodoma, kuna hela hapa, tafuteni hela zenu zipo Dodoma.” Amesisitiza Bw. Mmuya.

Aidha, Mkurugenzi wa Shirika linalosimamia mradi huo (CDIS) Bw. Daniel Leizer, amewashukuru Itracom kwa msaada wa mbolea hiyo ambayo itasaidia katika uzalishaji wa mazao, lakini pia amewashukuru kwa elimu waliyoitoa kwa vijana juu ya matumizi bora ya mbolea.

Naye Meneja wa Kampuni ya PARIJAT inayojihusisha na Uzalishaji wa viuatilifu Bw. Emmanuel Kiseke amesema kampuni yake imedhamiria kutoa msaada wa viuatilifu bora vyenye thamani ya shilingi Milioni 50 pamoja na mafunzo ya miaka mitatu kwa vijana wanaoshiriki kwenye Mradi huo ili kuwezesha na kujenga misingi imara ya kilimo chenye tija na endelevu.

Mradi wa Youth Enterpreneurship for Youth Food Agriculture (YEFA) una lengo la kuimarisha fursa za ajira kwa vijana kupitia kilimo cha mbogamboga na matunda unatekelezwa katika Mikoa ya Morogoro na Dodoma chini ya ufadhili wa AGRA ambalo ni Shirika linalojishughulisha na upatikanaji wa chakula Barani Afrika.



# MAAFISA HABARI WATAKIWA KUSHIRIKI TATHMINI NA UFUATILIAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Na. Hellen M. Minja

Maelekezo yametolewa kwa Makatibu Tawala na Wakurugenzi katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha Maafisa Habari wanashiriki kikamilifu katika ziara za Viongozi pamoja na timu za tathmini na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo ili waweze kuwa na uelewa wa kazi zinazofanyika na kuzitangaza.

Hayo yamebainishwa na Waziri wa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) Mhe. Mohammed Mchengerwa (Mb) alipokua akifungua kikao kazi cha Maafisa Habari wa Mikoa, Halmashauri na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo kinachofanyika kwenye ukumbi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Mtumba.

Lengo la Kikao Kazi hicho cha siku mbili kilichoanza leo Mei 23 – 24, 2025 ni kufanya tathmini ya pamoja ya utendaji kazi pamoja na kuhakikisha utekelezaji wa maagizo mbalimbali ya Serikali unafanikiwa kwa kuwashirikisha viongozi wa ngazi ya Mkoa, Taasisi na Halmashauri na Maafisa Habari hao.

“Hakikisheni Maafisa habari wanashiriki kikamifu katika ziara zote za viongozi pamoja na timu za tathmini na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo kwa lengo la kuwezesha kuwa na uelewa wa kazi zinazofanywa na Mikoa na Halmashauri ili waweze kuzitangaza kwani Maafisa hawa ni sehemu ya Timu yenu”. Mhe. Mchengerwa.




Aidha, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule ametumia kikao hicho kuwakaribisha Maafisa Habari hao ndani ya Mkoa wake sambamba na kumpongeza Mhe. Mchengerwa kwa kulikumbuka kundi hilo muhimu.

“Mhe. Waziri nikupongeze kwa kukumbuka kundi hili muhimu ambalo ndilo linafanya mambo mengi tunayoyafanya yafike Duniani na kwa Watanzania. Najua kwenye uandishi wa Habari kuna habari tofauti tofauti lakini kuna kulenga kuwa habari hii inalenga wananchi, Duniani huko au viongozi.”

Naye, Kaimu Katibu Mkuu TAMISEMI anayeshughulikia Miundombinu Mhandisi Rogatus Mativila, ametaja baadhi ya changamoto zinazowakabili Maafisa Habari nchini kuwa ni baadhi ya Mamlaka kuwatumia kwa kazi tofauti na walizosomea huku baadhi ya Viongozi wa Mamlaka kutowapa umuhimu wa kutembelea miradi mbalimbali ya Serikali.

Maafisa Habari wa Mikoa 22 pamoja na Maafisa Habari wa Halmashauri takribani 150 wamepata fursa ya kuhudhuria kikao kazi hicho kinachotarajiwa kuleta mabadiliko chanya kwenye Mamlaka na Taasisi zao pindi watakaporudi kwenye vituo vyao vya kazi.



# DODOMA YAJIANDAA KWA TUKIO KUBWA LA ZIARA YA MABALOZI MEI 27

Na. Hellen Minja



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule amefanya Mkutano na Waandishi wa Habari Mei 23, 2025 kwenye ukumbi wa Ofisi yake Jijini Dodoma ukiwa na lengo la kuutangazia Umma juu ya tukio kubwa la Kimataifa la ziara ya Mabalozi Mkoani hapa.Mabalozi hao ni wale wanaoiwakilisha Tanzania kwenye nchi mbalimbali Duniani,na wanaoziwakilisha Nchi zao hapa Nchini.

Tukio hilo litakalofanyika siku ya Jumanne Mei 27, linatarajiwa kuwa la kipekee ambapo Mhe. Senyamule ameelezea dhumuni hasa la ugeni huo.

"Dhumuni la kwanza ni kuweleza Waheshimiwa Mabalozi mambo yaliyopo katika Mkoa wa Dodoma na kuwa tuna huduma zote, wakiishi hapa; afya, elimu, miundombinu, maji, umeme na vitu vingine ambavyo vingemfanya mtu afurahie kukaa mahali, tunataka tuwaoneshe kuwa Dodoma huduma hizo tayari zipo na tunatamani waje sasa".

Aidha, Mhe. Senyamule amesema kuwa Dodoma ina vivutio vingi vya utalii na fursa za uwekezaji hivyo anatamani watu kutoka nchi mbalimbali duniani,zikiwemo ambazo mabalozi hao wanatoka,waje kuwekeza,kadhalika kuwaonesha kuwa Dodoma ni mahali sahihi na kuna fursa ya kufurahia utalii kama yalivyo maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Kadhalika, Mkuu huyo wa Mkoa amebainisha kuwa wanatamani Dodoma iwe na majina ya nchi za Kimataifa katika Mitaa kwani wanatamani Dunia ihamie Dodoma kwa kuwaambia Mabalozi fursa hiyo ambayo itawawezesha kufahamu maeneo kwa majina ya nchi zao kama vile mtaa wa Wachina, Wahindi na mingineyo ipatikane Dodoma.



Jambo jingine lililokusudiwa kwenye ziara hiyo ni kuwafahamisha wageni hao kuwa Dodoma ina Wilaya saba na Halmashauri nane ambazo zote zinahitaji kupata Miji rafiki kutoka katika nchi zao kwa ajili ya kubadilisha na uzoefu katika sekta mbalimbali ili kukwamua uchumi wa Mkoa kwa kushirikiana na watu wengine.

Ujio huo unatarajiwa kuhusisha kikao ambacho kitawaonesha na kuwapitisha mambo yote ya Mkoa wa Dodoma, baada ya hapo watatoka na kwenda kujionea mambo hayo wakianzia Hospitali ya Benjamin Mkapa, Mji wa Serikali Mtumba na kuishia Kiwanja cha Ndege Msalato.


Ziara hiyo imeandaliwa kwa kutambua mchango wa Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye amejenga mahusiano mazuri na nchi zote Duniani zinazowafanya wafurahie kuja Tanzania na haya yote wamekua wakiyafanya katika nchi mbalimbali hivyo sasa ni zamu ya Dodoma.

Kaulimbiu: "Dodoma ipo Tayari kwa Ajili yenu"

# FURSA ZA UWEKEZAJI KATIKA MKOA WA DODOMA.




Dodoma (makao makuu ya ya Nchi), inakua kwa kasi ya ajabu, ikijipambanua kuwa kitovu cha kibiashara na kiutawala cha Taifa. Fursa za uwekezaji katika sekta ya utalii na ukarimu hazijawahi kuwa nyingi namna hii. Uhitaji mkubwa wa hoteli za kisasa, kumbi za mikutano zenye uwezo wa kukaribisha matukio makubwa ya kitaifa na kimataifa, pamoja na huduma nyingine zinazohusiana na utalii, unazidi kuongezeka kila siku. Hii inatoa fursa ya kipekee kwa wawekezaji wenye nia ya kuingia katika soko hili lenye faida kubwa na mtiririko endelevu wa wageni wa ndani na nje ya nchi. Uwekezaji katika sekta ya ukarimu Dodoma utakuwa na faida ya muda mrefu kutokana na ukuaji endelevu wa uchumi wa Tanzania na ongezeko la shughuli za Serikali na biashara zinazoendeshwa katika Makao Makuu. Soko linahitaji hoteli za viwango mbalimbali, kuanzia zile za bei nafuu hadi za kifahari, kulingana na mahitaji ya aina mbalimbali ya wageni.



Aidha, fursa pia ipo kwa uwekezaji katika miundombinu inayosaidia utalii kama vile usafiri, maeneo ya burudani na vivutio vya utalii. Serikali ya Tanzania inatoa motisha mbalimbali za uwekezaji, ikijumuisha punguzo la kodi na ushirikiano wa karibu na wawekezaji ili kuhakikisha mafanikio ya miradi yao. Kwa wawekezaji wanaotafuta fursa za kipekee katika soko lenye ukuaji mkubwa na mtiririko endelevu wa mapato, Dodoma ni mahali pazuri pa kuwekeza. Ukuaji wa kasi wa mji unafuatana na ongezeko kubwa la wageni wa biashara, watalii na Watumishi wa Serikali, wote wanaohitaji huduma bora za malazi na mikutano. Uwekezji katika hoteli za kisasa na kumbi za mikutano hapa Dodoma utakuwa na faida kubwa kwa muda mfupi kutokana na uhitaji uliopo na uwezo mkubwa wa soko. Tunawaalika wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi kuja Dodoma na kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa Taifa hili kwa kuwekeza katika sekta hii yenye faida. Tunaamini kwamba uwekezaji katika Dodoma utakuwa na mafanikio makubwa kutokana na mazingira mazuri ya kibiashara, sera rafiki ZA uwekezaji, na msaada wa Serikali.Tunakukaribisha Dodoma, mji unaokua kwa kasi na fursa nyingi za uwekezaji zilizoko tayari kuwezeshwa. Karibu uwe miongoni mwa wawekezaji watakaonufaika na ukuaji huu wa haraka wa Dodoma.

# RC SENYAMULE APOKEA MABALOZI WANNE KUELEKEA 'DIPLOMATIC CAPITAL CITY TOUR' MEI 27

Na. Hellen M. Minja



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule leo Mei 26, 2025 amepokea ugeni wa Waheshimiwa Mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao hapa Tanzania ambazo ni Sweden, Denmark, Finland na Norway waliofika ofisini kwake Jijini Dodoma kufuatia tukio la ziara ya Mabalozi lililoandaliwa na Mkoa huu linalotarajiwa kufanyika siku ya Jumanne Mei 27.

Mabalozi hao wamefika Ofisini hapo kwa lengo la kujitambulisha na pia kupata taarifa za uwekezaji sambamba na vivutio vilivyopo Mkoani hapa kutokana na kushindwa kushiriki ziara iliyoandaliwa hapo kesho.

Akizungumza na Mabalozi hao, Mkuu wa Mkoa amewaeleza dhumuni hasa la kuandaa ziara hiyo;

"Wakati huu tumewaalika mje tuwaambie na kuwaonesha nini tunacho hapa Dodoma. Hatuwezi kutembelea sehemu zote kwa siku moja lakini nyinyi mnaweza kushawishi nchi zenu kuhamia Dodoma kwani Mihimili Mitatu ya Serikali yote ipo Dodoma hivyo ni wakati sasa wa kufikiria kuhusu uchumi wa Dodoma kwani Serikali imewekeza fedha nyingi kujenga miundombinu hapa."



Kadhalika, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma Dkt. Fredrick Sagamiko ametumia wasaa huo kuelezea juu ya Mradi unaotarajiwa kutekelezwa Hombolo kwa kuufanya kuwa Mji wa Kidiplomasia kutokana na uwepo wa Ziwa Hombolo ambalo lipo umbali wa Km 70 kutoka Dodoma Mjini na eneo hilo ni la kimkakati kwani lipo karibu na Mji wa Serikali, eneo la Mabalozi pia kiwanja cha ndege cha Msalato.

Ziara ya Mabalozi Jijini Dodoma imeandaliwa kwa kutambua mchango wa Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye amejenga mahusiano mazuri na nchi zote Duniani zinazowafanya wafurahie kuja Tanzania na haya yote wamekua wakiyafanya katika nchi mbalimbali hivyo sasa ni zamu ya Dodoma inakwenda na kauili mbiu ya "Dodoma Tupo Tayari kwa Ajili Yenu".

# TAWLA - SAUTI YA WANAWAKE NA WATOTO WALIOKOSA ULINZI WA KISHERIA KATIKA JAMII

Na. Hellen M. Minja




Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania, TAWLA, kimetajwa kuwa sauti ya Wanawake na watoto waliokosa ulinzi wa kisheria,ikiwa ni pamoja na kuchochea mabadiliko ya kisheria,kuondoa Sheria kandamizi zilizokua zinawakabili Wanawake na watoto ndani ya Jamii.

Hayo yamesemwa leo Mei 03, 2025 na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule wakati wa hafla fupi ya kusherehekea miaka 35 tangu kuanzishwa kwa Chama hicho iliyokwenda sambamba na uzinduzi wa jengo la ofisi yao Mkoani hapa lililopo eneo la Ilazo Jijini Dodoma.

"Natoa pongezi kwa kazi kubwa iliyofanywa na TAWLA ambapo mmekua sauti ya Wanawake na watoto waliokosa Ulinzi wa kisheria lakini pia mmechochea mabadiliko ya kisheria kwenye Sheria kandamizi, mmefanya tafiti zenye mchango mkubwa katika Sera, mmesaidia Wanawake, watoto na jamii kwa ujumla kupata elimu ya kisheria"

Kadhalika, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TAWLA Bi. Suzan Ndomba, amesema maendeleo ya Taifa hayawezi kufikiwa pasi na usawa wa kijinsia kwani Wanawake ni kiungo muhimu katika maendeleo, na nchi haiwezi kuendelea kama wasiposhirikishwa katika nyanja za Siasa, Uchumi, Elimu na Sheria.

Vile vile, Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba Wilaya Bi. Stella Tullo, ameongeza kuwa miongoni mwa kesi wanazozipokea kwenye Mabaraza hayo ni za Wanawake hivyo, wanapopata Wanawake ambao hawana uwezo wa kulipia huduma za Wanasheria, TAWLA imekua msaada mkubwa kwa Wanawake hao wakati wote.

Akizungumzia namna walivyopata ofisi hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa TAWLA Bi. Tike Mwambipile, amesema awali walikua na eneo lililopitiwa na Mradi wa SGR hivyo walilipwa fidia ya Milioni 42 iliyowezesha kupata eneo jipya la sasa ambapo walijenga ofisi na kuhamia rasmi 2024 na waliona ni vyema kulizindua rasmi katika sherehe ya miaka 35 ya Chama hicho.

Maadhimisho ya miaka 35 ya TAWLA yamekwenda sambamba na kauli mbiu za "Miaka 35 ya Haki na usawa" pamoja na "Haki haina jinsia" zote zikihamasisha na kutoa ujumbe kwamba utoaji haki hauchagui jinsia, kila mmoja ana haki sawa ya kupata msaada wa kisheria pindi anapouhitaji.

Na. Hellen M. Minja

# WAWEKEZAJI WA VIWANDA KUTOKA DUBAI WABISHA HODI DODOMA



Ikiwa ni siku moja tu baada ya ziara ya Kidiplomasia (Capital City Diplomatic Tour) iliyowahusisha mabalozi kutoka nchi mbalimbali Duniani Jijini Dodoma,Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule amepokea ugeni kutoka nchini Dubai kuzungumzia juu ya upatikanaji wa fursa za uwekezaji wa ardhi  kwa ajili ya kujenga viwanda kwa kuzingatia Dodoma inazidi kukua kutokana na hadhi yake ya Makao Makuu ya nchi na kupokea wageni wengi wa ndani na nje ya nchi.

Wawekezaji hao ambao ni Bw. Emmanuel Salinos na Bw. Walid Jumaa, wamefika ofisini kwa Mkuu wa Mkoa Jengo la Mkapa Jijini Dodoma Mei 28, 2025 ambapo hii ni mara ya pili kufika hapa kwa ajili ya dhumuni hilo ingawa awali waliona Dodoma haijakua kama ilivyo sasa.

Aidha, lengo hasa la wawekezaji hao ni kutafuta eneo lenye ukubwa wa ekari 1,000 kwa ajili ya kuwekeza na kutengeneza Mji unaofanana na Dubai ambapo wataleta wawekezaji wengine kutoka nchini mwao kwani wanaotaka kutengeneza eneo la uwekezaji wa Viwanda.

Mhe. Senyamule amewakaribisha Dodoma na kuwaambia kuwa ipo kwa ajili yao na pindi watakapokua tayari wakaribie huku akiwaeleza kuhusu ziara ya Mabalozi iliyofanyika Jijini hapa Mei 27, 2025 yenye lengo la kuwavutia kuwekeza.



“Jana tulikua na Mabalozi tukiwaonesha fursa za uwekezaji zinazopatikana hapa, na wameona maendeleo ya Dodoma ambayo hawakuyaona kabla. Kuna mpango wa Balozi zote kuhamia Dodoma kutoka Dar Es Salaam sasa,

Kila tunapowauliza lini mtakuja Dodoma wanasema bado hakuna huduma bora za afya, elimu lakini jana tuliwatembeza kwenye huduma hizo na tuna kauli mbiu ya ‘Dodoma tupo tayari kwa ajili yenu’ wameahidi kuzishawishi Balozi zao kujenga ofisi hapa”. RC Senyamule.

# KAMPENI YA 'GURUDUMU LA MAMA SAMIA' - MATOKEO YA IMANI YA SERIKALI KWA SEKTA BINAFSI

Na. Hellen M. Minja

Rais wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ametajwa kutengeneza mazingira rafiki kwa Sekta Binafsi kujenga imani kubwa kwa Serikali hasa linapokuja suala la mikopo ambapo kampuni ya 'Road Master' kupitia kampeni ya 'Gurudumu la Mama Samia' inakopesha magurudumu ya Pikipiki kwa gharama nafuu na kwa malipo kidogo kidogo.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule, ameyasema hayo leo Mei 28, 2025 alipokua akizindua Kampeni hiyo katika hafla fupi iliyofanyika kwenye viwanja vya soko la Machinga lililopo 'Bahi Road' Jijini humu ambapo magurudumu hayo yanakopeshwa kwa Maafisa usafirishaji wa Pikipiki maarufu kama Bodaboda.

"Sekta binafsi zimejenga Imani kubwa kwa Serikali kwa sababu ya dhamira ya Mhe. Rais kuwa yapo mambo ambayo yanatakiwa yafanywe na sekta binafsi lakini, ili sekta binafsi awe na Imani kuwa bodaboda nitawakopesha na kuwa amini kabla hajamaliza kulipa hela ni lazima itengeneze mazingira mazuri".





Kadhalika, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mhe. Jabir Shekimweri amempongeza Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini Mhe. Anthony Mavunde kwa kuendelea kujitoa kila wakati kusaidia wananchi wake kwani usaidizi huo, unakwenda kuokoa maisha na kuimarisha biashara za vijana hao siku za usoni.

Hata hivyo, Mbunge huyo amesema, kampeni hiyo imeridhiwa na Mhe. Rais kwa kuwagusa waendesha Bodaboda na Bajaji nchi nzima kwa kutambua changamoto kubwa waliyonayo ya upatikanaji wa matairi mapya kwa wakati, ikilenga kuwapunguzia mzigo vijana hao na mpango huo utaamsha ari ya vijana wengi kuzingatia sheria na kufuata taratibu hivyo kupunguza ajali za barabarani.



Naye, Mkurugenzi wa 'Road Master', Kampuni iliyoanzisha kampeni hiyo Bw. Fuein Makamba amesema kampuni yake imeitikia wito wa kumuunga mkono Mhe. Rais kupitia uwezeshaji wa haki za vijana hasa kundi la bodaboda na bajaji nchini kwani kupitia uwezeshaji huo, imeanzisha kampeni hiyo yenye lengo la kuchochea maendeleo ya vijana hao Mkoani hapa.

Kupitia Mpango huo, Afisa usafirishaji wa Bodaboda au Bajaji ambaye atahitajika kununua tairi mpya lakini hana fedha kwa wakati mmoja, kupitia mpango huo ataweza kutoa shilingi 10,000 akapata tairi mpya ya shilingi 70,000 na fedha iliyobaki atailipa kidogo kidogo kwa siku 30 awe amemaliza kiasi chote kinachohitajika.

# TIMU YA UMITASHUMTA 2025 MKOA WA DODOMA YASISITIZWA NIDHAMU, UPENDO NA KUJITUMA

Na. Hellen M. Minja

Wawakilishi wa timu ya Mkoa wa Dodoma kwenye Umoja wa Michezo kwa Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) 2025 inayotarajiwa kufanyika Mkoani Iringa, wametakiwa kuliheshimisha jina la Mkoa kwa kuwa na nidhamu, kupendana na kujituma ili kuhakikisha makombe yote yanarudi Dodoma.

Kaimu Katibu Tawala Msaidizi Seksheni ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mkoa wa Dodoma ambaye ni Afisa Elimu Taaluma Mwalimu Justin Machela, ameyasema hayo Mei 30, 2025 wakati wa hafla fupi ya kutangaza timu ya Mkoa itakayowakilisha kwenye mashindano hayo Kitaifa Mkoani Iringa iliyofanyika katika Shule ya Sekondari Dodoma.

"Makombe yanapatikana kwa namna tatu, kujituma sana uwanjani, nidhamu na kupendana ninyi kwa ninyi. Mkuu wa Mkoa anatamani kila tunaposhindana Dodoma tuwe wa kwanza kwa vigezo na viwango vya hali ya juu. Waalimu ambao tunakwenda na watoto, kazi yetu ni kuwasimamia na kuendelea kuwafundisha, kuhakikisha nidhamu ya watoto inakua juu na ya yetu pia inakua juu".



Kadhalika, Umoja wa Walimu Wakuu Tanzania (TAPSHA) ukiongozwa na Mwenyekiti wake Mwalimu James E. Manary, wameunga mkono juhudi za kuwawezesha watoto hao kukaa kambini kwa kipindi ambacho wanasubiri safari ya kuelekea Iringa kwa kutoa vyakula na fedha taslimu.

"Sisi vijana wa TAPSHA, tunakabidhi vitu vyenye thamnai ya shilingi 3,380,000 ambavyo ni vyakula, jezi za 'football' 22, jezi za 'netball' 10 lakini pia 'tracksuit' ambazo tumezitoa kama motisha kwa mtoto atakayefanya vizuri pia tunatoa fedha taslimu shilingi 730,000 ambazo 600,000 kwa ajili ya nyama na 130,000 ya vitafunwa".



Katika hatua nyingine, Afisa elimu awali na msingi Halmashauri ya Wilaya ya Chemba Mwl. Josephat Ambilikile, amezungumzia siri ya mafanikio ya Chemba kwani wamebeba vikombe vingi sambamba na kuibuka washindi wa jumla kwenye mashindano hayo ngazi ya Mkoa ambapo amesema ni ushirikiano mkubwa ulipo katika idara ya elimu Msingi na jitihada za Walimu shuleni.

Mashindano ya kutafuta timu ya Mkoa kwa ajili ya kushiriki UMITASHUMTA 2025, yameshirikisha wanafunzi 960 kutoka shule za msingi za Halmashauri zote 8 za Mkoa wa Dodoma ambapo mchujo ulifanyika na kupatikana wanafunzi 120 kwenye timu hiyo ya michezo mbalimbali ambao watakaa kambini hapo kwa siku 6 kabla ya kuelekea Mkoani Iringa.

# VITUO VYA 'KILIMO ANGA' NCHINI, KUPATA NDEGE MPYA ZA KUDHIBITI VISUMBUFU VYA MIMEA

Na. Hellen M. Minja

Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe, ametoa maelekezo kwa Watendaji wa Wizara yake kuanza mchakato wa ununuzi wa ndege mpya tatu kwa ajili ya vituo vya Kilimo Anga vya kanda vilivyopo katika mikoa ya Arusha,Mbeya na Mwanza lengo likiwa ni kudhibiti visumbufu vya mimea.

Maelekezo hayo ameyatoa wakati wa hafla ya mapokezi ya ndege moja ya kudhibiti visumbufu vya mimea iliyonunuliwa na Serikali chini ya Wizara hiyo kwenye Kiwanja kidogo cha ndege Mkoani Dodoma Mei 30, 2025 ambayo itatumika katika kituo cha Kanda ya Kati.

"Vituo vyote hivi vinatakiwa viwe vina ndege na 'drones' kwa hiyo, mchakato wa kununua ndege tatu nyingine uanze sasa hivi. Ni lazima kama Nchi ijitegemee, dunia ya kubebana haipo. Lazima tuweze kutoa huduma, tumeshaanza kununua 'drones' za kufanya 'survilence', mwaka huu tunanunua drone kwa ajili ya 'spraying'." Mhe. Bashe.


Kadhalika, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) Prof. Joseph Ndunguru, amesema ndege hiyo inalenga kuleta mageuzi makubwa katika Sekta ya Kilimo kwa kuleta tija, ajira na kupanua masoko lakini pia kuimarisha hali ya chakula hapa nchini na kuongeza kuwa visumbufu vya mimea ni moja ya jitihada za Mamlaka katika kuleta tija kwenye sekta hiyo.





Hata hivyo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe Rosemary Senyamule ameishukuru Wizara ya Kilimo kwa ununuzi wa Ndege hiyo ambayo italeta matumaini kwa Mkulima.

"Utashi huu unakwenda kuleta matumaini kwa Mkulima ambaye si mvivu, kwani amelima na kutunza mazao yake halafu mwishoni ndege anakula. Kwa Mkoa wa Dodoma itatuongezea upatikanaji wa chakula na wale wavivu sasa wataanza kulima kwani Dodoma pia tunapata athari ya Nzige maeneo ya Bahi na Kwelea kwelea maeneo ya Chemba, Kondoa na Kongwa."



Ndege hiyo aina ya 'Thrush 510 P2'iliyonunuliwa kwa gharama ya Shilingi 6,000,000,000 ina uwezo wa kukaa angani kwa zaidi ya saa 4 kutokana na tenki lake kubeba mafuta yenye ujazo wa lita 863, uwezo wa kubeba viuatilifu lita 1,930 uwezo wa kufanya udhibiti kwenye eneo la ekari 2400 kwa mara moja huku ikiwa na vifaa vya kisasa kwa ajili ya kutolea takwimu zinazowezesha mpango wa uthibiti wadudu na ndege waharibifu wa mazao na mimea.

# UBALOZI WA UINGEREZA NCHINI TANZANIA WAADHIMISHA MAFANIKIO YA MWAKA MMOJA NCHINI

Na; Happiness E. Chindiye

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary S. Senyamule Mei 08,2025 ameshiriki hafla ya jioni ya maadhimisho ya mafanikio ya mwaka mmoja tangu kufunguliwa rasmi kwa ofisi ya ubalozi wa Uingereza Jijini hapa na ushirikiano kati yao na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia ‘ Mutual Property Partnership (MPP)’ wenye lengo la kuimarisha biashara na maendeleo endelevu.

Tukio hilo lilofanyika kwenye Hoteli ya Collina Uzunguni Jijini Dodoma, limeangazia ushirikiano unaokua kati ya Serikali ya Uingereza na Tanzania wenye dhamira ya



pamoja ya kukuza maendeleo ya kiuchumi.

Hafla hiyo iliongozwa na Balozi wa Uingereza nchini Mhe. Marianne Young na kuhudhuriwa na viongozi ngazi ya Mkoa , Wilaya na maafisa kutoka Wizara ya Mambo ya nje.



## MNARA WA NYERERE SQUARE

Mnara uliojengwa kama kumbukumbu kwa lengo la kumuenzi baba wa Taifa Mwl. Julius Kambarage Nyerere hasa mchango wake katika harakati za kupigania uhuru wa Tanganyika. Mnara huu uliopo katikati ya Jiji la Dodoma, licha ya kuwa ikoni (icon) ya Mkoa wa Dodoma, pia ni eneo ambalo mara nyingi huwa na mkusanyiko wa watu wengi wakipumzika, kupiga picha na kuburudika.

Na; Happiness E. Chindiye

# MRADI WA KUIMARISHA HUDUMA ZA KIFAFA WAZINDULIWA DODOMA

Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma Bw. Kaspar K. Mmuya Mei 08,2025 amezindua mradi wa kuimarisha huduma za kifafa Tanzania (Enhancing Epilepsy Care Africa (EECA) ngazi ya Mkoa huu ambao utaenda kutekelezwa katika Wilaya za Chamwino na Bahi.

Uzinduzi wa mradi huo uliofanyika katika ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa unalenga kuanzisha mfumo endelevu wa huduma jumuishi kwa watu wanaoishi na kifafa Nchini.

Bw.Mmuya akizungumza na hadhira hiyo ametoa wito kwa Jamii kutowanyanyapaa Watu Wenye Kifafa kwa kuhakikisha wanapata stahiki zote za msingi kama watu wengine.

“ Kuanzia watoa huduma wasiwanyanyapae kadhalika kwenye Jamii watu wenye kifafa wapate haki zote za msingi kusoma, kupata ajira na huduma zote za kiafya” - Amesema Bw. Mmuya



Naye Meneja wa Mradi (EECA) Mradi wa kuimarisha Afya za Kifafa Dodoma Dkt. Dan Bhwana akizungumza wakati wa utambulisho wa mradi huo amesema utaendeshwa ndani ya mfumo wa huduma ya afya ya msingi ili kuhakikisha kuwa huduma hizi zitakuwa endelevu na kumilikiwa na jamii husika.



“Mradi huu unalenga kuongeza uelewa wa jamii kuhusu kifafa na kuvunja ukimya unaozunguka hali hii. kupitia kampeni za kupinga unyanyapaa na shughuli za kinga, tunatarajia kupunguza visa vipya vya kifafa na kuboresha maisha ya watu wanaoishi na hali hii,” amesema Dkt. Bhwana

Kampeni maalum za kuondoa unyanyapaa zitafanyika katika Wilaya za Bahi na Chamwino, sambamba na juhudi za kijamii za kuelimisha jamii kuhusu kifafa na kuboresha mapokezi ya huduma kwa kushirikiana na Wizara ya afya Magonjwa yasiyoambukizwa (NCDs), Ofisi ya Raisi Tamisemi na Pamoja na wadau wengine wa afya.

Na; Happiness E. Chindiye

# UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU AWAMU YA PILI:WANANCHI WA DODOMA WATAKIWA KUJITOKEZA




Wananchi Mkoani hapa wamesisitizwa kujitokeza kwenye uboreshaji wa daftari la kudumu la mpiga kura awamu ya pili utakaofanyika kuanzia tarehe 16 hadi 22 Mei, 2025 katika vituo vilivyo pangwa kwenye maeneo yao.

Hayo yameelezwa Leo tarehe 12 Mei,2025 na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary S. Senyamule wakati alipokutana na waandishi wa habari katika Ukumbi wa Mikutano wa ofisi yake, Jengo la Mkapa Jijini Dodoma.

“Nawasihi wanadodoma wote wenye sifa wafike kwenye vituo kuhakiki taarifa zao na kuendelea kufuatilia taarifa zinazotolewa na Tume huru ya uchaguzi “ - Amesema Mhe.Senyamule

Mhe. Senyamule amesema uboreshaji huo ni sehemu muhimu ya mchakato wa uchaguzi na unalenga kuhakikisha wapiga kura wote wanahakiki taarifa zao.

“Ni muhimu kwa wapiga kura kuhakikisha kuwa taarifa zilizopo kwenye daftari la kudumu la mpiga kura ni sahihi ili waweze kutimiza haki yao ya kupiga kura katika uchaguzi Mkuu wa mwaka huu 2025” - Amesisitiza

Hata hivyo Mkuu wa Mkoa huyo ameeleza uboreshaji huo utafanyika katika Mkoa wote huu ambapo idadi ya vituo kwa Mkoa mzima ni 413, huku idadi kwa kila Halmashauri ikiwa kama ifuatavyo;Chemba vituo 58, Jiji la Dodoma vituo 105, Kongwa vituo 41, Mpwapwa vituo 67, Bahi vituo 32, Kondoa Vijijini Vituo 44, Kondoa Mji vituo 16 na Chamwino vituo 50.

Aidha, Vituo hivyo vitakuwa katika Ofisi za Watendaji wa Kata ambapo kwa kata ambazo ni kubwa, utaratibu umeshafanyika, vituo vimegawanywa,hivyo kutakuwa na vituo kwenye ofisi za kata na katika maeneo mengine ambayo Wananchi watatangaziwa na Viongozi wao wa Kata, Mitaa/Vijiji.

Uboreshaji wa daftari awamu hii unahusisha kuandikisha wapiga kura wapya (wenye umri wa miaka 18 na kuendelea ambao hawajajiandikisha, na watakaotimiza miaka 18 kabla ya tarehe ya uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025), kukagua daftari, Wapiga kura kuhakiki taarifa zao, Kufanya marekebisho ya taarifa pamoja na kuweka pingamizi kwa wapiga kura wasio na sifa kuendelea kuwemo kwenye daftari.

Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma Bw. Kaspar K. Mmuya Mei 13,2025 ametembelewa na Wafadhili wa ‘Malala Fund’ ambao wanafadhili Shirika la Afyaplus linalotekeleza miradi iliyojikita katika huduma za maji na usafi wa Mazingira pamoja na uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Ugeni huo uliongozwa na Bi. Leila Seradj Mkurugenzi wa Ruzuku katika Mfuko wa Malala na Bi. Mary Qanita, Mkuu wa Wafanyakazi (Mwenyekiti Mtendaji) Bi. Jacqueline Raphael (Mratibu Miradi) pamoja na watendaji wengine wa Afyaplus.

Wakizungumza na Katibu Tawala ofisini kwake, Viongozi hao wa Mradi, wamesema mradi huo unalenga kuondoa changamoto anazokutana nazo mtoto wa kike katika safari yake ya masomo hasa wakati wa hedhi, ambapo tayari shule 20 katika wilaya tatu za Mkoa huu ambazo ni Bahi,Chamwino na Dodoma zimenufaika.

Mradi huu umeanzisha maabara za kushonea taulo za kike katika shule 10 za mkoa wa Dodoma, shirika limetoa Mashine za kushonea, vifungo, Overlocking pamoja na malighafi kwaajili ya kushonea taulo za kike,huku ukiendesha mafunzo ya hedhi salama pamoja na Afya ya uzazi katika shule 20 za mkoa wa Dodoma kwa kutumia mitaala ya Serikali.

# RC SENYEMULE ATUNUKIWA TUZO YA DR. SAMIA MWANAMKE KINARA KANDA YA KATI

Na; Happiness E. Chindiye




Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary S. Senyamule leo Mei14,2025 amekabidhiwa tuzo ya Mwanamke kinara Kanda ya Kati kutoka 'Central Women Connect, Mwanamke Kinara Awards' ambao ni waandaaji wa tuzo hizo,ambapo makabidhiano yamefanyika nje ya ofisi yake (Jengo la Mkapa).

Tuzo hizo za Dr. Samia Mwanamke Kinara, ni tuzo zilizoandaliwa kwa ajili ya kutambua nguvu ya mwanamke kwenye jamii. Zilitolewa tarehe 10/5/2025 katika ukumbi wa Lavenda Hotel Jijini Dodoma.

" Hii tuzo ni ya wanawake wote



wa Mkoa wa Dodoma ,twendeni tukaonyeshe kuwa Wanawake tunaweza, na kuwa mstari wa mbele kwa kuboresha taarifa kwenye Daftari la kudumu la mpiga kura ili tupate nafasi ya kupiga kura" - Amesema Mhe. Senyamule

Akizungumza kabla ya kukabidhi tuzo hiyo kwa Mkuu wa Mkoa,Mratibu wa 'Central Women Connect Mwanamke Kinara Awards' Bi. Rashida Mfaume amesema sababu za kumtunuku tuzo hiyo ya viwango vya juu na ambayo haishindaniwi, ni kutokana na heshima aliyonayo kama Mwanamke Kiongozi kwa kusimamia vyema miradi ya kimkakati.

"Kazi umeiendeleza katika sekta mbalimbali za maendeleo ndani ya Mkoa huu, zikiwepo usimamizi wa miradi, kuna ambayo imeshakamilika na mingine bado inaendelea, hivyo tunajivunia wewe, na unastahili kuwa mshindi wa tuzo hii". - Bi. Mfaume



Na; Happiness E. Chindiye

# WATANZANIA WATAKIWA KUILINDA NA KUIDUMISHA AMANI ILI KURUHUSU MAENDELEO NCHINI



Shime imetolewa kwa Watanzania kuendelea kuilinda na kuidumisha Amani iliyopo ili kuruhusu maendeleo yanayofanyika Nchini ambayo wakati mwingine huchukua muda mrefu kuyafikia.

Hayo yamesemwa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary S.Senyamule aliposhiriki maombi maalum ya kuliombea Taifa kuelekea uchaguzi Mkuu, yaliyoandaliwa na kanisa la Anglikana Parishi ya Msalato A . Jijini Dodoma.

Mhe. Senyamule amewataka Watanzania kudumisha amani hiyo kwa nguvu kubwa.

"Nchi yetu imeendelea kuwa na amani kutokana na misingi imara iliyojengwa na Mwenyezi Mungu mwenyewe kwa utashi mkubwa unaosimamiwa na Viongozi wetu tangu uhuru hivyo tuendeleze hii amani na utulivu. "

Naye Askofu Mkuu wa Kanisa la Anglikana Tanzania Dayosisi ya Central Tanganyika Dkt.Dickson Chilongani ameeleza malengo ya ibada hiyo ni kuomba amani na utulivu wakati wote wa uchaguzi, kuombea tume ,vyombo vya ulinzi na usalama , upatikanaji wa rasilimali zote zitakiwazo wakati wa uchaguzi , watu kujitokeza kupiga kura pamoja na kumwombea Rais .





Sambamba na hayo Mkuu wa Mkoa ametoa rai kwa Wananchi kushiriki kikamilifu kujiandikisha/kuboresha taarifa zao katika daftari la kudumu la mpiga kura ambalo pazia litafunguliwa rasmi kesho tarehe 16 hadi 22 mwezi huu.

Na; Happiness E. Chindiye

# WANAFUNZI WAHIMIZWA KUENDELEZA VIPAJI WALIVYONAVYO KWAKUWA NI FURSA YA AJIRA.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary S. Senyamule amewataka wanafunzi wa Shule za Msingi kutoka Halmashauri zote nane za Mkoani hapa ambao wapo katika kambi ya siku saba ya kuandaa timu itakayowakilisha Mkoa kwenye mashindano ya Umoja wa Michezo na Taaluma kwa Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) yatakayofanyika Kitaifa Mkoani Iringa kuendeleza vipaji walivyonavyo kwa kuwa ni fursa ya ajira kwa siku zijazo.

Wito huo umetolewa Mei 27,2025 wakati akizindua rasmi mashindano ya UMITASHUMTA ngazi ya Mkoa ambayo yanalenga kuunda timu ya Mkoa itakayowakilisha kwenye mashindano ya Kitaifa yatakayofanyika mkoani Iringa kuanzia Juni 08 mwaka huu.

" Mkoa wa Dodoma tunasema ni fahari ya Watanzania, tunataka isiwe kwenye elimu peke yake tunataka iwe kwenye mchezo na sekta nyingine zote.Hakikisheni kwa hii wiki moja mnajifunza vizuri ili mkatuwakilishe Kitaifa na mshike namba moja hivyo tumieni hii wiki vizuri Mkoa unatamani kuona matokeo haya,hauendi kwa ajili yako peke yako bali ni kwa Mkoa.

" Lakini ninyi kama wachezaji vipaji hivyo mkiviendeleza vizuri vinakuja kuwa ajira inakuwa ni faida yenu , ili iwe ajira lazima uonyeshe kipaji chako isiishie kwenye mdomo tu onyesha uwezo wako mkubwa kwa kujitofautisha na wengine ". - Mhe. Senyamule

Kwa upande wake Afisa Michezo wa Mkoa wa Dodoma Bw. Evance Sangawe pamoja na kueleza hali ya kambi hiyo ameainisha michezo mbalimbali itakayoshindaniwa na washiriki hao.

" Mkoa wetu wa Dodoma tuna programu ya vitalu ambapo kunakuwa na eneo maalum la kuandaa Wanafunzi kwa ajili ya mchezo ili kukuza vipaji huku mchezo ambayo tutashiriki ikiwa ni pamoja na Mpira wa mguu, Mikono, kwaya , na kadharika. " - Bw. Sangawe

Naye, Fatuma Jonas Mwanafunzi kutoa Shule ya Msingi Lamaiti kutoka Bahi akizungumza kwa niaba ya wenzake ambao wanashiriki mashindano hayo kutoka katika halmashauri za mkoa wa Dodoma ameeleza namna wanavyojiandaa ili wafanye vizuri katika mashindano ya Kitaifa.

" Tumejipanga vizuri kuhakikisha tunaenda kuwakilisha Mkoa wa Dodoma kwenye mashindano hayo ya UMITAMSHIMTA mkoani Iringa kwa kurudi na ushindi mkubwa kwani michezo ni mingi hivyo tuna imani tutashinda"




# POLISI DODOMA WAPONGEZWA KWA KUWA MSTARI WA MBELE UHAMASISHAJI MATUKIO YA KITAIFA

Na Sofia Remmi

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe.Rosemary Senyamule tarehe 19 Mei 2025,amefunga bonanza la michezo katika uwanja wa Mtekelezo Jijini Dodoma lililoandaliwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Dodoma kwa ajili ya kuhamasisha wananchi wajitokeze katika uboreshaji wa daftari la kudumu la mpiga kura.

Akizungumza wakati wa hotuba yake, Mhe. Senyamule amelipongeza jeshi hilo kwa kuwa mstari wa mbele kuanzisha kampeni za uhamasishaji pindi yanapotangazwa mazoezi ya Kiserikali.

“Ni mara ya Nne kushiriki hamasa zinazotolewa katika mabonanza yanayoandaliwa na Jeshi la polisi. Kila yanapotokea matukio ya Kitaifa mmekuwa nafasi ya mbele kuanzisha michezo ya kampeni inayoendana na matukio hayo. Ninawapongeza kwa kampeni hii ya uchaguzi salama unawezekana, kwa kuleta hamasa kwa vijana na jamii kwa ujumla ili kuwaunganisha Wanadodoma na Watanzania kwa ujumla kufanya uchaguzi wa amani”amesema Senyamule.

Kwa upande wake Kamanda wa polisi Mkoa wa Dodoma SACP George Katabazi amesema michezo inasaidia kupunguza uhalifu katika mkoa wa Dodoma na hii kampeni tumeianzisha ili kuzuia na kutokemeza uhalifu kwa vijana.

“Tumeanza michezo hii na polisi Jamanii,na imekusanya wachezaji kutoka kata 14 za Mkoa na michezo hii imeenda sambamba na kuelimisha kujitokeza katika kujiandikisha katika Daftari ka Kudumu la Mpiga kura na kushiriki kujitokeza kupiga kura” Amesema katabazi

# RC SENYAMULE AFUNGUA MAADHIMISHO YA KITAIFA YA SIKU YA NYUKI DUNIANI.

Na Sofia Remmi




Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mheshimiwa Rosemary Senyamule, amefungua Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Nyuki Duniani leo tarehe 18 Mei 2025 katika Bustani ya Mapumziko ya Chinangali ( Chinangali Park) Jijini Dodoma.

Akizungumza na wananachi pamoja na wadau wa Nyuki Mhe. Senyamule amesema Dunia nzima huadhimisha Siku ya Nyuki ambayo ni matokeo ya makubaliano ya Baraza la Umoja wa Mataifa mnamo Mwaka 2017.

Lengo kuu la kuanzishwa kwa madhimisho haya ni kutambua mchango wa Sekta ya Nyuki katika maisha ya mwananchi mmoja mmoja, Taifa na Dunia kwa ujumla,Siku hii ni sehemu ya kuenzi jitihada za mwanzilishi wa ufugaji Nyuki Bwana Anton Janša raia wa nchi ya Slovenia ambapo Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa ziliidhinisha na kutangaza rasmi tarehe 20 Mei ya kila mwaka kuwa siku ya Nyuki Duniani itakayoadhimishwa na kila Nchi Mwanachama wa Umoja huo kulingana na mazingira ya Nchi Husika.

Mhe. Senyamule amesema kwa mwaka huu maadhimisho haya yameanza rasmi tarehe 17 na kilele chake kitakuwa tarehe 20 mwezi Mei 2025 katika Viwanja vya Chinangali.

“ Wafugaji nyuki, wajasiriamali na wafanyabiashara wa mazao ya nyuki na wadau wengine wa sekta ya Ufugaji Nyuki hukutana kwa lengo la kujengeana uwezo wa namna bora ya kuendeleza Sekta ya Nyuki katika Mkoa wa Dodoma na Nchi Yetu kwa ujumla.

Wadau wote wa sekta hii tunapaswa kuyatumia maadhimisho haya kikamilifu ili tuweze kujiinua kiuchumi na kuiendeleza Sekta ya Ufugaji Nyuki.

Mkoa wa Dodoma una zaidi ya mizinga 18,000 ya nyuki yenye uwezo wa kuzalisha zaidi ya kilo 135,000 za asali”Amesema Mhe. Senyamule.

Kwa upande wake Kamishna wa Polisi Benedict Wakulyamba,ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii amesema Nyuki amekuwa ni Muhimu sana kwenye maisha ya Mwanadamu, anastaili kuitwa kiumbe nyuki kwasababu ya kazi zake.

“ Umuhimu wa kiumbe huyu, ametambuliwa siyo tu kwa binadamu hata kwenye maandiko ya vitabu vya Mungu yametaja sifa za kiumbe nyuki.Tunapojivunia maendeleo ya sekta ya nyuki hatuna budi kutafakari kuhusu uendelevu wa sekta hii kwa ujumla”amesema Wakulyamba.

Maadhimisho hayo yameenda sambaba na kaulimbiu isemayo “Nyuki kwa Uhai na Uchumi Imara, tuwahifadhi”.





Na. Sizah Kangalawe

# MAAFISA MAZINGIRA WAPEWA HEKO NA RAS MMUYA

Wataalamu wa mazingira Wilaya za Mkoa wa Dodoma, wamepongezwa kwa juhudi mbalimbali wanazofanya katika kuhakikisha Usafi, ubora na utunzaji wa mazingira unadumishwa na kuendelezwa Mkoani hapa.

Pongezi hizo zimetolewa na Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma Bw. Kaspar Mmuya, wakati akifungua kikao kazi cha mapitio ya mpango kazi wa mazingira wa kila Halmashauri, kilichofanyika Mei 6,2025 katika ukumbi wa Mikutano wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Jengo la Mkapa.

''Naendelea kuwapongeza wataalamu wote wa Mazingira kutoka katika Halmashauri zetu, ninafahamu kazi nyingi mnazofanya katika kusimamia mazingira. Siwezi kuainisha moja moja najua mna mambo mengi ambayo mnayafanya kudhibiti uchafuzi wa mazingira ambao unaweza kuathiri udongo, vyanzo vya maji, na hewa.

Aidha Mmuya amewahamasisha Maafisa hao kuendelea kutoa Elimu juu ya utunzaji wa mazingira pamoja namna sahihi ya kutenganisha taka kwa aina zake.

''Sasa hiyo yote ni katika kutoa Elimu, tusafishe mazingira yetu na tuwe na uwezo wa kutenga taka, na tuwe na uwezo wa kuzidhibiti vizuri. Kwahiyo ninawashukuru sana kuwa nyie ndio wasimamizi wa kitaalam katika Halmashauri zetu".

Kikao hicho kinafanyika kwa usimamizi wa Maafisa viungo wa Mkoa wa Dodoma kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais na kinawajumuisha Maafisa mazingira, Maafisa Maliasili wa Wilaya, pamoja na Maafisa mazingira na Afisa Afya wa Mkoa.

# BILLIONI 14 KUJENGA OFISI ZA UBALOZI WA UGANDA JIJINI DODOMA.

Na. Sizah Kangalawe

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule Mei 09/ 2025 ameshiriki hafla ya uwekaji jiwe la msingi ujenzi wa ofisi za ubalozi wa Uganda Nchini, zinazojengwa katika mji wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma.

Akizungumza na washiriki wa hafla hiyo Senyamule ameweka bayana kuwa ujenzi wa ofisi za Mabalozi Jijini Dodoma unatokana na uwepo wa miundombinu rafiki inayotekelezwa na Serikali ya awamu ya Sita Chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

''Ni baraka kubwa kwetu kama Mkoa, kuona watu wameielewa Serikali kuwa Dodoma ndio makao makuu, na wameamini hata wao wa ngazi za Ubalozi na diplomasia wanaweza kuishi Dodoma,hilo ni jambo la faraja kwetu.

"Hii yote inatokana na uwekezaji wa Serikali uliofanywa na Rais wetu ambaye amewekeza fedha nyingi, sio tu kwenye mji wa Serikali lakini huduma mbalimbali zinazowarahisishia kufika Dodoma, huduma nzuri za afya pamoja na ujenzi wa Uwanja wa ndege wa kimataifa Msalato ambao utawawezesha mabalozi kutua Dodoma moja kwa moja kutoka nchi mbalimbali", amesema Senyamule




Kwa upande wake Balozi wa Uganda nchini Tanzania Mhe. Kanali Fred Mwesigye ameeleza kuwa ujenzi huo si tu jengo la kuhudumia wananchi bali ni kituo muhimu cha kuimarisha na kukuza zaidi uhusiano wa kiuchumi na kidiplomasia baina ya Tanzania na Uganda.

Aidha Balozi mwesigye amesema Uganda inaona fahari kutumia fursa hiyo kuwa nchi ya kwanza kuanzisha ujenzi wa Ofisi ya Ubalozi ikiwa ni sehemu ya kutoa shukrani zake kwa Serikali ya Tanzania kwa mchango iliyoutoa katika ujenzi wa Taifa la Uganda.

Hata hivyo RC Senyamule ametumia fursa hiyo kuzihimiza Balozi zingine zilipo Nchini, kuhamishia ofisi zao Jijini Dodoma, kwa kuwa Serikali tayari imeshaweka mazingira rafiki na wezeshi ya kuwawezesha kutekeleza majukumu yao vyema wakiwa Jijini hapa.

ujenzi wa Ofisi za Ubalozi huo utagharimu zaidi ya billioni 14 za Kitanzania na unatarajiwa kukamilika ndani ya miaka miwili.



Na. Sizah Kangalawe

# DODOMA NA DHAMIRA YA DHATI YA KILIMO CHA TUFAA (APPLE).

Ni matamanio ya viongozi kuona uchumi wa Wananchi wanaowaongoza unaongezeka kwa kasi na unakua wa kuridhisha hususani katika pato la Mwananchi mmoja mmoja na eneo husika.

Uongozi wa Mkoa wa Dodoma Ukiongozwa na Mhe. Rosemary Senyamule, unayo matarajio, matumaini, nia na dhamira ya dhati ya kukuza pato la wananchi wa Mkoa huu pamoja na pato la Mkoa kwa ujumla wake.

Ili kuyafanikisha hayo Mkoa umeanza jitihada mbalimbali za kuhakikisha ndoto na nia zao za dhati zinatimia ikiwa ni pamoja na kufanya tafiti mbalimbali za kitaalamu juu ya nini kinaweza kuwakwamua wananchi wake kutoka katika wimbi la umaskini na kuwa katika uchumi wa kati hadi uchumi wa juu.

Mkoa wa Dodoma umedhamiria kuanzisha kilimo biashara cha zao la tunda maarufu la tufaa (apple) kwani kutokana na utafiti uliofanyika, zao hilo linaweza kustawi katika ardhi ya Dodoma na likaleta matokeo ya kuridhisha.

Ili kufanikisha kilimo hicho Mkoa umechukua jitihada mbalimbali ikiwemo kusafiri umbali wa zaidi ya KM 310 kutoka Dodoma - Ifunda, Mkoani Iringa katika Shamba la Tamu Tamu Tanzania, mahali ambapo uzalishaji wa Miche ya tufaa pamoja na bidhaa mbalimbali zinazotokana na tunda hilo unafanyika.

Lengo la ziara hiyo ni kujifunza kwa vitendo namna kilimo hicho kinavyofanyika kitaalamu pamoja na kujifunza namna sahihi ya kuendesha kilimo hicho, ikiwa ni pamoja na kujua aina zinazostahimili hali ya hewa ya Dodoma, mbolea na viuatilifu vinavyostahili n.k.



Akizungumza wakati wa Ziara hiyo, Mhe. Senyamule amesema '' Tumekuja hapa na tumejifunza, tumehamasika na tumepata ari kuwa kumbe mawazo yetu, yanaweza yakawa ni mapinduzi ya kiuchumi kwa wananchi wa Mkoa wa Dodoma hasa uchumi wa Mwananchi mmoja mmoja.

''Sisi leo tumekuwa ni watu wenye furaha sana kuwa tunaanza kuona ndoto tunayoifikiria kwa ajili ya wananchi wa Dodoma, tunayoiona Dodoma ya Miaka 5 ijayo, tunaona watu wenye furaha, Uchumi lakini sisi kuzalisha tu bali tuanzishe na viwanda vya kuliongezea thamani zao hili, soko bado lipo nchini na nchi za wenzetu pia", amesema Senyamule.

Aidha Mhe. Senyamule ameweka bayana maazimio ya ziara hiyo kuwa ni pamoja na zao hilo kuwa miongoni mwa mazao ya Mkoa, kuanzisha kilimo hicho kabal ya 2025 kumalizika, kila Halmashauri kuanzisha shamba darasa kuanzia hekari 1 yenye miundombinu ya umwagiliaji pamoja na kuwapeleka maafisa ugani wa wilaya kupatiwa mafunzo juu ya zao hilo.

Akizungumza kwa niaba ya Wakuu wa Wilaya, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mhe. Alhaji Jabir Shekimweri amekiri unafuu wa uzalishaji wa zao hilo ukilinganisha na mazao mengine ya kibiashara yanayolimwa Mkoani Dodoma.

''Zao hili la Tufaa (Apple) gharama zake za uzalishaji ziko chini ukilinganisha na shamba la zabibu, kwaiyo sisi kama Wilaya tumeichukulia ziara hii kwa uzito unaostahili na sisi kama Jiji tayari tunayo maeneo tuliyoyatenga ya kuanzia uzalishaji wa zao hili ambalo tunatarajia ndio litakalo kuwa mbadala au ziada ya Zabibu", Mhe. Shekimweri

Ziara hiyo ya siku moja iliwajumuisha Viongozi wa Mkoa (Mkuu wa Mkoa na Katibu Tawala Mkoa), Wakuu wa Wilaya , Wakurugenzi, Wataalamu wa kilimo pamoja na wadau wa kilimo wa Mkoa wa Dodoma.

Na. Sizah Kangalawe

# VIONGOZI WA DINI WASISITIZWA KUHUBIRI AMANI.



Viongozi wa Dini Mkoa wa Dodoma wamesisitizwa kuendelea kuliombea Taifa pamoja na kuhubiri Amani kwa waamini wa Dini mbalimbali wanazoziongoza.

Rai hiyo imetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule Mei 14,2025 wakati wa kikao na Viongozi wa Dini wa Mkoa wa Dodoma, Kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi yake Jijini Dodoma.

‘’Tunamshukuru sana baba wa Taifa kwa historia, alipotujengea ule umoja hadi mtu unajiuliza aliwezaje? kitu kikubwa kilichofanikisha hili ni ile tuongee lugha moja, lakini pia namna mikoa ilivyogawanywa.Baba wa Taifa alisema kabila moja lisikae Mkoa mzima peke yake, ndio maana utagundua kila Mkoa una kabila zaidi ya moja.



‘’Mwaka huu tunazo chaguzi, nyakati hizi tutasikia maneno mengi masikioni mwetu kwasababu katika chaguzi sio wote wanadhamira njema, lakini tunachowaomba Amani ya Nchi yetu ipewe kipaumbele na umoja wetu wa Kitaifa upewe kipaumbele’’, Mhe. Senyamule

Hata hivyo Mhe. Senyamule ametumia wasaa huo kueleza juu ya ujio wa Siku ya Samia (Samia day) ambayo itakuwa ni siku maalum ya kuelezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita, ambapo siku hiyo itaazimishwa kwa kata zote za Mkoa huu.





# ZAIDI YA BILIONI 11 ZILIVYOWANUFAISHA WANUFAIKA WA TASAF DODOMA

Na. Sizah Kangalawe

Billion 11,123,585,402.18 zimetumika kuwalipa wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya masikini (TASAF) kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Takwimu hizo zimetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma,Mhe. Rosemary Senyamule wakati akifungua kikao kazi cha tathmini ya utekelezaji ya mpango huo.

‘‘Serikali ya awamu ya 6 kwa kushirikiana na wadau wengine inaendelea kutoa fedha nyingi kwa ajili ya TASAF ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi April 2025, Mkoa umepokea Tsh. 11,123,585,402.18 kwaajili ya kulipa walengwa, usimizi na ufuatiliaji wa Mpango.

Kadhalika,Mhe. Senyamule amesema Serikali inaanda mpango mzuri wa kuzitambua kaya hizo ‘‘Ni matarajio ya Serikali kuwa katika tathmin ijayo walengwa wengi watakuwa wamekidhi vigezo ili kutoa nafasi kwa walengwa wengine kunufaika na mpango huu katika awamu nyingine zinazokuja”, Mhe. Senyamule

Hatahivyo Mkuu wa Mkoa huyo amewaagiza wataalam wa Halmashauri kuendelea kutoa elimu ya ujasiriamali na usimamizi wa miradi kwa walengwa wanaonufaika na fedha hizo ili zitumike kuanzisha miradi ya kiuchumi itakayowaongezea kipato.

Kwa upande wake Mratibu wa Tasaf Mkoa Bi. Josephine Paschal ametaja njia zinazotumika kuwalipa fedha wanufaika hao,ambapo kuanzia Julai hadi Aprili 2025 kaya 45,771 zimenufaika. Kati ya hizo, kaya 26,275 sawa na 57% zimelipwa fedha mkononi, na kaya 19,474 sawa na 43% zimelipwa kwa njia ya benki na simu ( E- pay) lakini Msisitizo wa TASAF ni kuhakikisha kaya zote zinalipwa kwa E- Payment”, Amesema Bi. Josephine

Aidha Bi. Josephine amesema kupitia Mpango huo kaya 45,771 za Walengwa, wamepatiwa mafunzo ya Ujasiriamali yanayotolewa na wataalam katika kila dirisha la Uhaulishaji huku lengo likiwa ni kusaidia kaya hizo kuibua miradi midogo itakayowawezesha kuongeza kipato chao.

# WAKANDARASI WASIOKAMILISHA MIRADI KUDAIWA FIDIA

Na. Sizah Kangalawe

Waziri wa Ujenzi Mhe. Abdallah Ulega, amewataka Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS) na Taasisi nyingine zinazosimamia ujenzi wa miradi ya Serikali, kuwatoza faini wakandarasi wanaochelewa kukamilisha miradi hiyo baada ya mikataba yao kumalizika, ikiwa wameshapatiwa stahiki zao zote.

Agizo hilo limetolewa na Waziri huyo wakati wa ziara yake ya kikazi ya kukagua miradi mbalimbali inayotekelezwa na Wizara hiyo kupitia kupitia TANROADS Mei 21/2025 Jijini Dodoma.

‘’Hakikisheni tunawadai kwasababu sisi tumekuwa tukidaiwa kwenye miradi yetu pindi tukicheleweshа jambo, kwahiyo inapotokea wao wamechelewa ni lazima na wao watulipe sisi kwa muda ambao wamechelewa, kama msumeno vile, unakata pande zote kwetu na kwao.

Aidha Mhe. Ulega ameitaka TANROADS kushirikiana kwa karibu na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) ili kurahisisha utendaji kazi kwani baada ya kumalizika kwa ujenzi huo Mradi utakabidhiwa kwa TAA.

‘’TANROADS na TAA mpo hakikisheni mnashirikiana kwa karibu kufanya hii kazi, hili jambo ni la Watanzania wote, ni kweli kazi ya ujenzi tumepewa sisi TANROADS na Mikataba yote lakini TAA ndio watumiaji na Watanzania wote, TAA akiona uzito wa mambo ninyi msimfungie milango kuona kwamba hawezi kutoa ushauri, msukumo. Inawezekana kuna jambo atakaloliona yeye kama mtumiaji , msimamizi wa baadae mradi ukikamilika, mkifunga milango atashindwa kuwashauri kitaalamu”, Ameagiza Ulega




Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule amewaomba Wizara ya Ujenzi kwa kushirikiana na TRC kujenga njia ya mchepuko ya muda ili kuwezesha bandari kavu kuanza kufanya kazi yake kama ilivyokusudiwa wakati ujenzi wa barabara kuu ukiendelea.

Ziara hiyo imehusisha kutembelea barabara ya mzunguko wa nje kutoka Ihumwa – Matumbulu na Matumbulu- Veyula ambapo ujenzi wake unatarajiwa kukamilika kati ya Julai 31 na Agosti 30/2025, Ujenzi wa Uwanja wa ndege wa kimataifa Msalato ambao utakuwa na uwezo wa kusafirisha abiria Milioni moja na laki tano kwa mwaka pamoja kuwa na uwezo wa kuegesha ndege 17 kwa wakati mmoja.

Hata hivyo miongoni mwa maagizo yaliyotolewa katika ziara hiyo ni pamoja na wakandarasi kufanya kazi usiku na mchana ili kukamilisha miradi kwa wakati na kuzingatia mahitaji ya watumiaji wadogo wa barabara pindi wanapojenga barabara ya juu ( Fly over) katika makutano ya barabara ya juu ya mzunguko wa nje Mtumba, jijini Dodoma.

# MMUYA AHIMIZA UDHIBITI VIFO VYA MAMA NA MTOTO.

Na. Sizah Kangalawe

Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma Bw. Kaspar Mmuya Mapema Mei 26/2025, amepokea taarifa ya awali ya kazi ya utafiti uliofanyika kwenye Mkoa wa Dodoma kati ya Februari 17 – Mei 11/ 2023 katika Halmashauri za Bahi, Chamwino na Mpwapwa.

Utafiti huo umefanyika kwa ushirikiano wa Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), OR- TAMISEMI, Wizara ya Afya na Taasisi ya Ifakara Health Institute ikiwa ni kutekeleza utafiti wa kufuatilia ugonjwa wa Malaria Tanzania bara kwa kutumia mbinu za vinasaba.

Akizungumza katika hafla hiyo Mmuya amewataka waatalamu hao kuhakikisha wanatokomeza kabisa vifo vya mama wajawazito na watoto walio chini ya Umri wa miaka 5.

''Muangalie sana eneo la watoto wadogo chini ya miaka 5, Mimi nazungumza kwasababu nina 'Interest', nyie wote mnafahamu Mhe. Rais anavyopambana na vifo vya akina mama na watoto,. ndio maana yake kuwa ni lazima tuwalinde hawa, katika utafiti wetu tuangalie kama tunaweza kuwalinda akina mama wajawazito aidha wakipata au wasipate Malaria ni kitu gani tukifanye hawa wawe salama pamoja na watoto waliowabeba", amesema Mmuya





Kwa upande wake Mratibu wa Utafiti huo Prof. Deusdedith Ishengoma amesema wamepanga kufanya tafiti katika zahanati 3 zilizopo Mkoani Dodoma, kufanya mafunzo wezeshi vituoni, pia ameweka bayana kuwa wanatarajia kukamilisha zoezi la utafiti huo ndani ya miezi 2- 3.

Waliofika kuwasilisha utafiti huo ni Prof.Deusdedith Ishengoma, CPA Obedi Olekaondo na Bi Priscilla Mlay kutoka taasisi ya Ifakara Health Institute (ihi)

# UHAKIKI ANUANI ZA MAKAZI KUANZA MEI 28 DODOMA

Na. Sizah Kangalawe




Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma Bw. Kaspar Mmuya amewataka Wakurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha wanasimamia kwa ukamilifu zoezi la uhakiki wa taarifa za anuani za makazi, linalotarajia kuanza Mei 28/ 2025 katika Halmashauri za Mkoa wa Dodoma.

Mmuya amesema hayo wakati wa uzinduzi wa zoezi la Uhakiki wa Taarifa hizo Mei 26/2025, Katika ukumbi wa Mikutano wa Four point Hotel Jijini Dodoma, uliowahusisha watendaji kata, wenyeviti wa Serikali za mitaa na vijiji na Maafisa Tarafa.

‘’Wakurugenzi wote, hakikisheni mnasimamia zoezi hili katika halmashauri zenu huku mkitambua kuwa ni zoezi endelevu hivyo sitegemei kusikia mmeacha kuhuisha taarifa baada ya siku za zoezi hili kumalizika.

‘’Vilevile hakikisheni mnatumia Mfumo wa anuani za makazi kutambua makazi na wakazi katika maeneo yenu ili kuongeza ufanisi katika kusimamia mazoezi mbalimbali ya kitaifa na kupanga mipango ya maendeleo”, Amesema Mmuya

Akitoa salamu za Jiji la Dodoma Meya wa jiji hilo Prof. Davis Mwamfupe amesema Jiji hilo limejitanabaisha kuwa Jiji nadhifu na litakalokuwa mfano kwa kutoa huduma bora.

‘’Uhakiki huu tunaokwenda kuufanya unakwenda sambamba na ukweli kwamba Dodoma tumejitanabaisha kwamba ni mji nadhifu , sio kwa maana ya usafi tu lakini ‘Smart City’ ambayo sasa utoaji wa huduma lazima uwe katika kiwango cha juu” ameweka bayana Prof. Mwamfupe

Baada ya uzinduzi wa zoezi hilo kutafanyika mafunzo ya siku mbili kwa viongozi wa Serikali za mitaa na kata ya kuwawezesha kufanya zoezi hilo katika ubora unaotakiwa na zoezi la uhakiki litafanyika kwa siku 12 kuanzia tarehe 28/05/2025.

Zoezi la uhakiki wa anuani za Makazi, linafanyika chini ya uratibu wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kushirikiana na wataalamu wa ngazi ya Mkoa na Wilaya.



**Jarida hili limetolewa na:**

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma.

Pakua jarida la FAHARI YA DODOMA kupitia
www.dodoma.go.tz

Dodoma Region

mkoa_wa_dodoma Mkoa wa Dodoma _dodoma.go.tz